Msimulizi, 1894[1]

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission station of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The perodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1894.

MSIMULIZI. 1894
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa,"

MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam, illi wa baada ya salaam, habari ni hizo nakuletea. Mwezi Nov. 1893, pametuasilia Padre G. Dale, na Shemasi Kisby huyu sahibu yake sana Padre Grindrod: wote

[1] The text is issued under licence CC BY-NC

hawa wawili wameenenda pande za Magila. Mwezi Dec. ametuasilia Frederick Mwakusega amekuja fanya kazi Hospital, mahali pa nduguye Mattayo.

Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana hatukuenenda popote siku kuu zote tumeshinda papa hapa. Siku ya Dec. 28 - tumepata huzuni sana kwani Stephen Shante, aliyerudi Kongo juzi juzi amefariki baada ya ugonjwa wa siku chache tu.

Dec. 29 - palikuja wanaake wa Mbweni kutazama mchezo mtakatifu uitwao kwa Kiingreza "Sacred Play of the Incarnation" kama ile mingine ichezwayo huko na huko, lakini huu ni Mtakatifu.

Wakumbuka, kana katika Msimulizi wa 31 ukurasa wa 705, soma, utaona habari za Uganda, ya kuwa vita ilisaki, bassi Dec. 30, 1893, barua zalitujia za kumaliza habari. Sikia bassi, vita ikawa nzito hatta wale walio wajinga wapiganao pasipo kujua sababu vema, shughuli yao ilikuwa kuzunguka vichaka na kurudia mjini na huenda kuwaangukia miguu ndugu zao illi wawasamehe, huwatolea bunduki & viembe vyote, ishara ya kutubu. Na wale waliokimbilia Unyoro. Ah! baba, makubwa hayo, kwani sikia walipotokea tu inchi ya Unyoro, jumbe akapelekwa, Amani! Amani bwana! twaja tukimbilie inchi yako. Sababu yenu ya kukimbia? Ah! ah! kunde, mbazi hazijaiva, Akawaambia, Je! Mwaka jana mwalinitendeaje? (Kwani walifanya vita kubwa

MSIMULIZI. 723

sana kati ya Wanyoro & wao) na leo mwaja kwangu siwatakeni hatta kidogo. Marra mbiu ya vita ilipigwa, Ah! wache Waislamu wafyate mkia, kwani wamechoka ati, watapiganaje? Huku wafukuzwa na huku wafukuzwa, bassi, wakajimwaga tu katika nyika, wawili huko, mmoja huko, watatu huko, hatta siku hizi wanarudi Uganda; wakitokea mwituni mmoja mmoja, wakienenda kuwaangukia miguu ndugu zao. Na wangine wakifika sio kutubu tu, lakini huongoka na huingia katika dini yetu. Bassi siku hizi amani yazidi. Kwani juzi hapa wamewasili watu watokao huko huko, hunena vita hapana illa tauni ya nzige tu. Nzige wameingia katika inchi wazito mno ajabu, hatta nafaka hamna mashambani imesalia njaa tu, hithara ya pili ndio, wale wadudu wa Kongo wamejaa huko, hatta hapana tofauti tena ya wadudu kati ya Kongo & Buganda, wamesaki hatta wametapakaa inchi yote.

Mwezi Jan. siku ya kwanza ya mwaka mpya, tulienda kushinda hapo penyi shamba la serkali paitwa Sebuleni, tukajifurahisha hapo kama tuwezavyo, mnamo alasiri kasiri tukashuka zetu mjini. Usiku wake uleule, watoto wa Sagara ndio watoto wa nyumba ya kazi ya Mr. H. Lister, walikarimiwa riziki ndio chayi, matunda na mpunga wake pia, aliyewakarimu ni Padre wetu mkubwa. Daktari, walikuja masahibu wengi awafahamuo, illi kushariki riziki. Siku hiyo mchezo wa tinge ulisimamishwa mpaka mnamo saa tano hivyo.

Siku iliofuata watoto wa Kiinua Mguu waliwasili hapa jioni, illi kutazama ule mchezo mtakatifu. Siku ya Alhamisi watu wa hapa Mkunazini wakaonyeshwa mchezo Mt. na ndio mwisho wa kuchezwa pia.

Usiku huo huo, palikuwa na ajabu ingine huko Mnazi mmoja, ndio mchezo wa Ulaya Amerika, Australia

MSIMULIZI. 724

ao tunene kwa jumla mchezo wa inchi za Uzunguni kwani huo si mchezo tu, lakini maarifa yapitayo kuneneka, waitwa kwa Kiingreza "Circus" (ulizia Mzungu ukaaye naye - atakuelezea labda.) Maarifa hayo siwezi kueleza, kwani si kitu kimoja wala viwili ati, umeona mtoto wa miaka 5 akichezeshwa kwa nyayo ya miguu kana pia? Ao umeona bibi akipanda mwanzi usio na tawi? na huo mwanzi umewekwa juu ya bega la mtu? Bassi ni hayo na zayidi ya hayo watu walioleta mchezo huo ni Wazungu na Wasina kuambiwa sikuona baba, heri ungekuja kuangalia illi uthubutishe. Habari zake tele zipo lakini siwezi kueleza maarifa hayo kwani ni "Unyakoga" huo.

Ndipo ikawa zamu ya watu wa hapa kuangalia mchezo Mt. kwani mwenyi mchezo alipenda kwanza kuwakaribisha wageni wa mbali kwanza, na mwishowe ndio wenyeji na ndivyo kwenenda.

Wajua kana Jany 6, ilikuwa siku kuu ya Epifania bassi watoto wa hapa walikwenenda Mbweni kwa mkutano uliokuwako wakafurahi, wakaturudia mnamo jioni kwani zilitumika mashua siku hiyo.

Panapo Juma a pili ya pili ya Epifania sisi hapa tumepatikana na huzuni ndio mtoto mmoja wa chuoni amefariki jina lake Rufo Changua, tulimzika Jumaa tatu Ziwani. R.I.P.

Labda utapenda kujua kama ndugu waliosafiri barra wangine wamerejea George Kambwende karejea akitoka mlima Kenia & Kilimanjaro. Tena P. Mlanzi karejea akitoka Buganda, wangine wengi wako huko huko nje.

Wakumbuka katika Msimulizi wa No. 27 ukurasa wa 621, Balyozi mkubwa wa hapa alitumwa Buganda, bassi akaenenda akafanya kazi yake, kama alivyoweza, baada

MSIMULIZI. 725

ya hivyo akafunga safari yake ya Ulaya Ingreza illi kusudi akawapashe habari yote akafika kwao, salama, wallakini panapo mwezi huu Jan. 23, 94 simu imekuja Unguja yanena Balyozi Portal kafariki. Bassi baba kwa sababu naye ni mtu, baba, fortha zote zilifungwa hapana kupakia wala kupakua mzigo wowote. Ikawa kimya tu. Ndio habari.

Bwana Askofu amewasili akitoka barra Newala pamoja naye Luka Lichinga na mtoto mwingine mgonjwa wa macho, jina lake Kibwana, ni mtoto wa mfalme Che Mtarika amempeleka kule Newala asome, lakini sasa yupo hapa auguzwa macho. W. E. K.

MASASI.

Tumesikia kama mwaka huu chuo cha huko Masasi kimeongezeka sana watoto, wapata zayidi ya sittini; bassi furaha kubwa sana kusikia kama chuo kinaendelea vizuri. Hatta mnaosimamia hamtoshi mwatafutia waalimu wangine Kiungani, haina buddi kuwasayidieni mkitaka waalimu ndio furaha sana ndugu kazi yetu izidi kuendelea.

Tena tumesikia kama huko Masasi habari njema tena si njema tu illa kwa kuwa ninyi wote wazima kwa rehema za Muungu.

Mbaya kwa kuwa tumesikia kama panapo December 18, habari za vita ndio watu wa Mkonona ng'ambo ya Ruvuma walikuja kwa mfalme jina lake Mkuti, kutaka kuwasayidia kwani wanaonewa sana na Mangoni, watu wakaao upande ule. Bassi tumepata habari kama karibu Masasi yote ikaenda vitani kwa wale Mangoni. Jumla bunduki zilikuwa 200 tulioyasikia na ngao 50, hawa wenyi ngao ndio watu watawalao Masasi yote huitwa Makwangwara wanaotoka mbali sana magharibini. Bassi

MSIMULIZI. 726

tulivyosikia vita ilitoka Dec. 21, na Wamasihiya wengi sana walikwenda katika vita hii. Lakini tumesikia tena kama vita hii haikuwahi kufika mjini kwani vyakula vyao vyaliisha upesi. Nussu wakarudi na nussu wakaendelea mbele, lakini wale wenyi kuwaajiri watu hawa wa Masasi, wakatoroka. Bassi nao hawakuwa na buddi kurudi kwao wakarudi.

Tena tumesikia kama siku kuu hii ya Kuzaliwa ilikuwa furaha kwa watoto hatta wamecheza nussu mwezi ndizo Jumaa tatu kamili.

Tumesikia kama Askofu aliwasili Masasi mwezi Jan. 4, na baada ya kukaa siku kumi na moja, amefunga safari yake kurudi tena huku Unguja: Mtg.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu. Natia mkono katika karatasi kukupasha habari kidogo tu za huku kwani mwalimu Kolumba, na Luka Lichinga ajaye kumleta mtoto mgonjwa kwa Doctor Palmer, watakupa habari zote za hapa. Wallakini mimi nitaweza kukuambia machache tulivyocheza sikukuu yetu.

Siku yenyewe ya Christmas palikuwa na shangwi sana, watu 150 wakashariki. Mr. Hood ameleta hapa vastment vyeupe vizuri sana, tena kaleta Banner nayo pia nzuri. Tena Juma apili iliyofuata ikatumiwa chalico mpya aliyoleta huyohuyo Mr. Hood, kwa ukumbusho wa Babaye, haikuweza kutumiwa Christmas kwa maana ilichelewa kuja, nzuri sana imejaa mawe ya thamani sana, uzuri wake umepita chalice zote nilizoziona mimi. Juma nne baada ya Christmas ndio ukawa mtawanyiko. Luka, Leonard na Kolumba wakaenda Rovuma, nami nikafunga safari pamoja na Askofu kwenda kwa Machemba. Tulitoka Juma nne alasiri, tukaenda kulala kwa Msusa.

MSIMULIZI. 727

Assubuhi tukafika Chitangali tukala chakula tu tukapita, tukaenda kulala karibu kwa Namaleche, assubuhi kama saa a tano tukawasili mjini. Mwenyewe hatukumkuta alikuwa shamba marra tulipofika hakukawia marra akarudi. Siku hiyo hiyo Askofu akaanza kumweleza habari aliyoijua, lakini hatukusema vema siku hiyo kwani palikuwapo mtu mlevi akifanya kelele na kurandaranda. Bassi Askofu hakupenda kusema neno pamoja na mlevi tukaagana, jioni akaja tena na watu wachache tu, ndiyo tukaongea vizuri. Naye Machemba kwanza alikataa kabisa kupeleka watu kwa Wadachi kutaka kupatana. Lakini halafu akakubali, lakini kukubali kwake hakuna hakika, kwani watoto wengi hawakuwapo; bassi sithani kama wao watakubali shauri hili. Machemba alituheshimu sana wala hawakutufanyia uthia wowote, alimpa Askofu mbuzi na taka 5 za nguo kusudi tununue wenyewe mbuzi, tukakaa kama siku mbili. Ijumaa tukatoka, alasiri, Juma amosi Chitangali, nami nikakaa juma nzima, Askofu akaniacha kwenda Masasi.

Padre Cecil alinikaribisha sana. Baada ya juma nikawasiri hapa Newala. Mfalme mmoja akaaye juu ya Rovuma, jina lake Namagono, amekuja hapa kutembea, na kufanya mashauri na mzee Matola. Mwalimu Luke anakwenda kukaa Masasi kwa kitambo mpaka aje mwalimu mgine, kwani watoto wanazidi kuwa wengi na Mwalimu ni mmoja tu. Safari ya Rovuma imerudi imefanikiwa sana, kwani wameua nyama wengi. Chipolopolo alikwenda Mtamba kwa Wareno kuuliza kama waje Makwangwara kuwapiga Wangoni, kwani wanauthi mno watu siku hizi, yeye Chipolopolo alifuatana na mfalme Namiundu kwani yeye mji wake umepigwa na hao Mangoni, akaja kushitaki kwa mzee Matola. Na wakati huo Chipolopolo yupo hapa, bassi alipopata

MSIMULIZI. 728
habari hizi akasema, nikirudi nitamwambia Sonjea tulete vita kuwapiga hawa Wangoni. Lakini Matola alimwambia ukitaka vita itafaa uende kwa Wareno kuwaarifu kwanza, kwani Wangoni hawa wanaofanya uthia ni wa ng'ambo ile ya Rovuma, na ng'ambo ile ndiyo miliki ya Wareno. Bassi akaenda na huyu Namiundu, amerudi leo, alivyojibu Mreno hatujasikia bado. S. C.

CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu.

Nov. 30, akatuwasilia Bwana Askofu toka Unguja pamoja na Bwana Cook mwalimu wa Newala, tuliposikia kama yupo mtoni anapikia chakula cha saa sita, mzee Barnaba Nakaam akapeleka watu waende kumlaki, wakamsalimu kwa bunduki nyingi watu wakacheza ngoma usiku kwa kumshangalia, naye alishinda kama siku sita hapa. Na ile siku ya 30 ya Nov. ndio siku yake mwaka wa 10 tangu alijitoa kwa kazi hii ya Mission. Na Bwana Cook hakushinda hapa ussubuhi mapema akatoka kwenda zake Newala, naswi ussubuhi ya pili hatukusoma tukapewa siku nzima ya kucheza.

Dec. 1, akaenda Askofu kwa njia ya Miwa kwenda Newala akamchukua mwalimu Yustino kupita kusudi amsayidie njiani kwani aliwapitia wafalme wawili awaone, ndio maana akamchukua mwalimu Yustino.

Dec. 10, palikuwa na Ubatizo wa watoto wawili wachanga mmoja babaye Mmasihiya na mamaye Mwanafunzi na mmoja amefiwa na mamaye, bassi wanaomtunza sasa ndio Wamasihiya Isaak Sasu na Sarah Sasu wakamwomba Padre abatizwe.

Dec. 11, mwalimu Rose alienda Masasi amwone mwalimu Harry na mkewe, na ussubuhi yake ikawa shughuli ya

MSIMULIZI. 729

kuwatazamia watoto wa chuoni, jumla ya mambo waliyojifunza nuss mwaka huu, ikachukua siku 2, na siku ya tatu ikawa kupumzika kwa watoto.

Dec. 12, Padre alienda Newala, awasikie watu wa kule kwa maneno ya Kiyao watarajio kujiweka tayari kwa siku kuu ya Kuzaliwa.

Dec. 19, Tulienda Newala mimi na mwalimu Daniel na Carlo, maana Bwana Askofu aliwataka waalimu wote wa pande hizi wakusanyike Newala kwa faragha ya siku moja, na Alhamisi ussubuhi kunako saa 8 ndio killa mtu akawa anaenda kwake, sisi tukawasili hapa kunako kama saa 9. Juma a mosi hatukupamba, maana majani yetu yamekuwa thaifu mno mwaka huu. Tukahofu kunyauka, bassi ikawa Juma a pili alasiri mapambo yetu. Na jioni ikawa Sala kuu kwa Wamasihiya na Waanafunzi na Wasikia pamoja na mahubiri. Ussubui kunako siku kuu yenyewe saa 10 za usiku wakatoka Waalimu hawa na watoto wote wajuao kuimba hatta njiani wakapiga bunduki za kuwastusha watu, walipokiamka wameisha anza kuimba, wakaimba wahadi ussubui. Kwanza walienda nyumbani kwa mzee Barnaba Nakaam, tena nyumbani hapa Misison, tena wakaenda kulizunguka kanisa. Panapo saa 1 kassrobo zikaanza kengele marra Kanisa limeisha jaa watu. Kwani huja Waanafunzi kwenyi Ush: Mt. wahadi penyi Imani wanatoka, na watu waliosharikiwengi. Kwenyi saa 4 kathalika watu wengi wakaja, na jioni kathalika. Jioni yake ndio ikawa matezo ya Lingaka na ngoma ya Kinyassa wahadi ussubui, wakaacha, tulipoisha Sala wakaingilia tena wahadi saa 6 ngo! ngo! bassi mchana huu aliye fundi ndipo akajulikana, alitokea kijana Mwanafunzi, aitwa Kunde, Yee alifungwa mpikoni na kitwa chini bassi akawa amechukuliwa mithili mahamali wanavyochukuzana kasha wawili, akipiga ngoma yake,

MSIMULIZI. 730

bassi wakamshangalia mno akapewa zawadi kubwa sana. Kunako Kinyassa alitokea Mwanafunzi naye aitwa Feruzi, yee ndio alikuwa akitwangwa mithili wanavyotwanga watu mchele, na haya yalikuwa yakitendeka mchana saa 5 unussu.

Dec. 27, Askofu alitokea hapa kama saa 4 akienda kumwona mfalme Machemba pamoja na Mwalimu Samwil Chiponde. Dec. 29, nikatoka kwenda Masasi ikawa taabu kwa saa 2, maana tukapita njia ya Miwa nikashinda siku 4; nikarudi kwa njia ya Mwiti nikamkuta Padre Mwiti, kwani alikuwa na Bwana Askofu na wakati huu Askofu ameisha enenda Masasi tukawa tumekosana njia. Ussubui Jan. 5, tukang'oa na Padre wahadi hapa Chitangali saa 8 kassrobo. Mwiti ni jina la mto na mto ule ndiko alikohamia Mzee Maluchila ndugu wa Mzee B. Nakaam, na mashamba ya mto huu yanaota sana tumbako, bassi wanapanda sana huko, na waliolima kandoni kabisa, mihindi maboga &c wanaweza kupata nyakati zo zote, wala si wakati wa mvua tu. Jan. 1, tukafungua School yetu kuanza tena kusoma maana tuliifunga kwenyi siku kuu ya Tomaso. Safari hii Askofu anawachukua Waalimu 2 ndio Danieli Usufu na Carlo E. Lisomba wanarudi tena Kiungani kusoma, kwani walituwasilia Nov. 2 kuja kuwaangalia wazee wao; na mwaka huu imekuwa shidda sana huku kwetu kwa kupata mvua, maana ni desturi yetu kuanza kupata mvua mwezi wa Nov. mwisho, ao mwanzo wa Dec. kunako siku kuu ya Uzaliwa vyakula vimeisha mea, lakini mwaka huu sio, hatukupata mvua wahadi mwanzo wa Jan. na watu waliopanda kwa kawaida ya killa mwaka wamepanda kama marra mbili. Wamasihiya na waanafunzi walikusanya mbegu zao Kanisani zibarikiwe mbele ya siku kuu ya Uzaliwa.

Jan. 17, Tumepatwa na msiba maana ndugu yetu

MSIMULIZI. 731

mmoja Haruni Boli amefiwa na mwanawe ameugua kama siku tatu tu, amefariki na maungo yake pasipo kukonda.

Jan. 20, amewasili Bwana Askofu akitoka Newala aenda zake Unguja kwa njia ya Machemba. A. K.

MBWENI.

Kwa mtengenezaji wa Msimulizi salaama, baada ya salaamu, nakuarifu habari zipitazo hapa petu.

Dec. 21, Siku kuu yake Mtume Tomaso hatukwenda mahali twalikaa petu hapa, alasiri tukacheza kwa shamba la Balyozi.

Dec. 25, Kuzaliwa Bwana wetu, kama saa ya kwanza, kwa desturi ya siku kuu siku zote, ndipo twalienda kanisani, na watu waliojaliwa kujiweka tayari, walikwenda pokea Chakula kile cha roho, nao ni themanini na tano.

Dec. 26, Siku kuu yake Stefano twalijifurahisha na walakini hatukwenda popote.

Dec. 27, Siku yake Yohana Mwanjilisti, siku hii twalikarimiwa mno na bibi yetu Miss Thackeray, kwani alituchukua katika Shamba lake tukashinda kule na killa mmoja alionekana kufurahi.

Dec. 28, Siku yao Wasiokosa hatukwenda popote. Twalijifurahisha na michezo yetu tu.

Dec. 29, Jumaa twalikaribishwa karibu watoto wote wakubwa Mkunazini kutazama mchezo Mtakatifu, killa mmoja wetu alionyesha ginsi alivyopenda mchezo wenyewe.

Jan. 1, Tohara ya Bwana wetu, twalikaa hapa hapa, hatukwenda mahali.

Jan. 5, Twalitengeneza nyumba yetu tayari kupokea wageni toka Kiungani na Mkunazini.

MSIMULIZI. 732

Jan. 6, Siku ya Wonyesho tulipata wageni wengi wengi weusi kwa weupe, alasiri killa moja akarejea kwake.

Jan. 13, Juma a mosi, Balyozi mdogo alitukaribisha nussu yetu kutazama mchezo Mnazi mmoja, tuliupenda mno, hatta hatukuchoka kuutazama.

Jan. 18, Hapa Mbweni palikuwa na mchezo, walikaribishwa watu bali si wengi sana. Nao mchezo ni huu:

(l) Beauty and the Beast, (2) Maisha yake Agnes Mt., tena watoto wa Mwalimu Connie wakaimba, twalipenda sana kuimba kwao; tena mwisho ikawa chakula kidogo, na baada ya chakula wageni wakaenda zao.

Jan. 25, Kuongoka Mtume Paolo hatukwenda pahali, tukajifurahisha na michezo mingine mingine.

Jan. 20, Huzuni nzito sana mno iliyotuangukia hapa Mbweni, Ee! ndugu zetu, tumefiwa na bibi yetu mpenzi

Miss A. M. GAY.

Amekaa naswi kama miezi mitatu tu, aliugua homa yake ya kwanza na ndio iliyomtwaa. Alionekana bibi mwenyi upendo kwa killa mtu, na hodari pia. Homa yake ilimwanza Jan. 10, Juma tano, Juma apili iliyofuata kaonekana amezidi, bassi wakaona heri apelekwe Hospial. Huko akalala, siku hiyo hiyo assubuhi mapema mwili wake ukaletwa hapa, assubuhi ile ukafanywa Usharika Mt., mchana wote tukaenda zamu kwa zamu, kuulinda mwili wake, panapo alasiri, tukaenda mazikoni watu wengi waliokuja kwa maziko yake. R. I. P. K. Sh.

HABARI ZA KIUNGANI.

Salamu kwa huu mwaka mpya, nami sijui kama safari hii mtakaribishwa na watu wengi, kwa sababu wananiona kama mzee; kumbe bado sijawa mzee, ni mzalia mimi

MSIMULIZI. 733

wa Unguja. Labda nitakuja kuwa goboleni (mzee), lakini bado mimi ni seneda (kijana), tu.

Nami siku hizi naumia kwa njaa, kwa sababu wale Waletaji habari zangu mimi Msimulizi, siku hizi wananinyima, wala si wote wanaonilisha kwa habari zao.

Bassi baada ya salamu yangu nawaarifuni habari zangu za hapa kwangu nipigwapo mimi (chapa si bakora!) ndizo hizi:

Dec. 20, Mwalimu Benedict Madalito naliwaambieni kama alienda Mrima Dare-Salam, bassi panapo siku hii alituasilia tena.

Dec. 23, Juma amosi, ikatulazimu kupunguza kazi zetu tayari kwa siku kuu ya Uzaliwa tukapamba nyumba yetu na Kanisa kwa majani ya miembe tu. Hatta panapo saa tissia unussu tukashika matembezi.

Dec. 24, Juma a pili, tulipokwisha kutoka Kanisani sala ya assubui; tukakaa kidogo hatta ilipotimu saa tano marra killa mtu akatafuta kikapo kuchumia maua. Kiisha ndipo tukaanza kumaliza kupamba kwetu, na bendera na taa pia.

Jioni yake, marra kengele zikapigwa, ndipo ikaanza sala ya shangwi, tukalizunguka Kanisa ndani tukiimba "Carols," na tukatolewa khutuba, baadaye sala zikaisha.

Usiku killa mtoto aomba mchana uwe, wapate kufurahiwa kwa siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu. Marra ilipopiga tu saa kumi, na majogoo ya kwanza yalipokianza kuwika; marra moja pasipo kukawia tukaamka tukapanda darini tukaimba nyimbo za Uzaliwa (Christmas Carols) mpaka kulipopambazuka tena kumekuwa kweupe, tukashuka, na killa mtu akajitengeneza tayari kwa sala kuu ya Kimasihiya.

Saa kwanza kengele zikapigwa, tukaingia Kanisani wa shangwi kubwa, na bibi Miss A. M. Gay ndiye

MSIMULIZI. 734

aliyetupigia kinanda, na watu wengi walioshariki siku hiyo. Halafu saa nne ikawa sala ya Assubui.

Dec. 26, tulikaa papa hapa, wallakini panapo saa tatu tukapewa zawadi killa mtu akafurahi. Siku hiyo hiyo ikafungwa mizigo tayari ya kwenenda kushinda Mkokotoni, Archdeacon Jones-Bateman na Wazungu wawili, na watoto thelathini na moja, ndio waliokwenenda, na habari zao ndizo hizi:

Dec. 27, Juma atano, safari yetu tukatoka hapa panapo saa kumi na moja, tukaenda mpaka Bububu: pale tukapumzika kwa hitaji la kufungua vinwa vyetu, na kuwangojea wapagazi maana walibakia nyuma yetu, wapagazi walipowasili marra tukaanza safari yetu, tukashika njia moja kwa moja mpaka tukafika pahala panaitwa Chichele; nasi tukatumaini tutapata chakula cha athuuri. Na mahali hapa tulifika mnamo saa nne, bassi, tukawangoja wapagazi hatta mmoja asitokee, bassi, tukawa watu wa kushangaa, tufanyeje? tukawa watu wa kutazamana tu, na wangine wamejinyosha. Wazungu wakanunua madafu matatu wakanywa, Archdeacon akamwambia mwalimu Cyprian H. Chitenje ya kwamba atangulie na watoto chache wapitie bandari ya Mwanda wanunue mchele; bassi wakatoka, na sisi wangine wakatuacha hapa Chichele. Walipofika Mwanda wakamwendea Mhindi awakopeshe fetha wanunue mchele watangulize Mkokotoni, maana wapagazi walichelewa kutukuta. Lakini Mhindi alikataa kabisa, akawaambia, nawajuaje nyinyi! fetha zangu zikipotea je! Bassi wakashindwa wakawa hawana buddi kwendelea kituoni, na sisi kule nyuma tukakaa mpaka saa kenda unussu pale Chichele wala wapagazi wasitokee hatta mmoja. Bassi tukatoka pale na njaa yetu tukijikokota pole pole, lakini njia yetu ilikuwa rahisi kuliko yao wale waliotangulia. Bassi tukafika saa edashara

MSIMULIZI. 735

unussu, tukapanda kilima mpaka juu kabisa ilipo nyumba yetu tukapumzika, marra tukawaona wenzetu waliopitia Mwanda wanakuja, tukawa na furaha tukitumaini labda wamechukua mchele, kumbe tukawaona mikono mitupu. Tukawauliza, habari? wakajibu, Mhindi amekataa kutukopesha fetha kabisa. Ah! Watu wote marra tuliposikia vile, tangu Wazungu pia tukalegea. Archdeacon akamwambia mwalimu Cyprian achague watoto wapendao wafuatane naye mpaka kwa Nokoa; wakapatikana watatu, wakamwendea Nokoa, jina lake Bwana Abudu. Archdeacon alipomwarifu ginsi tulivyothii kwa njaa. Marra Bwana Abudu kwa nguvu zake zote akahimiza watu wawili kuwafuata wapagazi wetu maana hatta sasa hawajatufikia. Akaandika barua akampa mtu mmoja, akaenda nayo haraka mpaka Mwanda, watu wangine wakatuangulia madafu mengi, na watu wangine wakachukua vyungu kupeleka kituoni petu. Tukarudi kule kilimani, kukaa dakika tano tu twamwona mtu aliyekwenda Mwanda amechukua kikapo cha mchele, marra hiyo tukajipa nguyu tukapika, tukala, tukapata nguvu. Tena panapo saa kwanza ya usiku tukawaona wapagazi wakija.

Dec. 28, Alhamisi siku kuu yao Wasio na hatiya, assubui ukafanywa Usharika Mt:, tena mchana wa siku ile tukawa watu wa kutembea-tembea tu. Jioni Archdeacon, akasema ya kwamba kesho mnamo saa kumi majogoo ya kwanza tutashika njia ya kurudi.

Dec. 29, Alfajiri mapema tukatoka tukaenda weee hatta tukafika mahala pana mwembe na kisima papo tukatua illi kupumzika. Tena tukaambiwa kama, watakao kutangulia watangulie. Bassi wangine tukatangulia tukaenda mpaka Bububu, tukaanguliwa madafu killa mtu kwa shibe yake. Tena tukashika njia ya Kiungani, tukafika wawili wawili, wanne wanne, maana tumechoka, wangine wakafika

MSIMULIZI. 736

saa saba, wangine saa tissa, na wangine jioni kabisa. Ndizo habari za Mkokotoni thaifu mno. Lakini siku ile watoto wa chuoni tulipokwenda Mkokotoni, watoto wafanyao kazi nao walienda kisiwa cha Makaburi na jioni yake wakarejea usiku.

Jan. 2, Tulienda Mkunazini kuangalia mchezo mtakatifu, Jan. 4, Mackenzie Meweawa amesafiri Mamboya kwenda kuwapikia Wazungu kule. Siku ile ile jioni tulikarimiwa mno na Mr. Boustead kwenda wote pia usiku hatta Mnazi Mmoja kuangalia Machezo ya Ulaya Amerika na Australia, haswa na tunene kibin Adamu ni machezo ya Uzunguni, Kiingreza yaitwa "Circus", machezo hayo yalitufurahisha kupita cheo. Illa, Ebu mmeona wapi frasi akiamrishwa kama bin Adamu, akiweza kufahamu aamuriwavyo, lala, hulala, amka, huamka, kimbia hukimbia, nipe mkono humpa. Tena tumeona mtu akisimama juu ya kamba na kukimbia, tena nyani anayefahamu anayoambiwa tena mtoto mdogo kama wa miaka mitano akidakwa-dakwa na kuzungushwa kama pia kwa unyayo wa miguu tu. Yapo mengi balli ni vigumu kueleza bora uone mwenyewe kwa macho. Hatta ilipotimu saa sita usiku machezo yakaisha, tukarudi.

Jan. 6, Siku ya Epifania ya Bwana wetu, tulitoka hapa saa nne unussu kwenda Mbweni, maana ni siku ya mkutano, na watoto wa Mkunazini pia walikwenda. Tulikaribishwa vizuri sana, hatta jioni killa mmoja akarudi katika masikani yake.

Jan. 7, Miss R. Berkeley alikuja kukaa hapa kwa juma moja, maana Wazungu wote walikuwa hawawezi billa Archdeacon tu.

Jan. 18, Watoto nussu tuliitwa usiku kwenda Mbweni kuangalia mchezo, tulipenda, kiisha tukarudi. Jan. 19, Darasa ya pili mpaka ya nne walitazamiwa akili zao

MSIMULIZI. 737

Examination, kwa siku mbili unussu. Jan. 20, Tulipata habari ya huzuni kama yule Bibi Miss A. M. Gay amefariki R. I. P. Ikawa msiba mkubwa kwetu, tukimkumbuka kama Siku ya Uzaliwa alitusayidia kwa upendo wake kwa kutupigia kinanda, Yuko wapi? Hatumwoni, ameitwa na Baba yetu wa mbinguni, astarehe katika taabu za dunia hii mbaya. Siku hiyo hatukusogea popote tulikaa papa hapa, na ilipopiga saa kumi tukaenda Mbweni kwa maziko watu wengi sana waliokuwapo. Jan. 25, Siku ya Kuongoka Paolo Mt., hatukuenda popote.

Jan. 30, Tumempeleka ndugu yetu Lawrence Mmaka kwenda Bonde kuanza kazi yake ya kufundisha. Jan. 31, Bwana Askofu amewasili Unguja, pamoja na watoto watatu walioenda tazama jamaa zao, ndio mwalimu Daniel Usufu, Carlo E. Lisomba na Yohana G. Mpalila, na mkewe Cyprian H. Chitenje jina lake Rose Rebeka. Feb. 1, Ametuasilia Mwalimu Archibald A. Semmanyi pamoja na mkewe, wanakaa hapa.

Siku ile ile panapo saa nne unussu za ussubui, zikanenwa habari za Examination. Bassi katika darasa ya pili aliowatangulia wangine, 1. Francis Sapuli, 2. Isaya F. Mwalinjila.

Katika darasa ya tatu wa 1. Yustino Dodo, 2. Edward T. Koongani; na katika darasa ya nne wa 1. Guy Dawnay Ngumbi, 2. John Kasimbwa. Labda wangine watastuka kwanini darasa ya kwanza haikunenwa, sababu yake ndio, maana Waalimu wengi hawakuwapo, walisafiri kutazama jamaa zao, lakini sasa wamerudi, na twatumai huenenda ikawapo.

Feb. 6, Jioni ilikuwa faragha (Retreat) kwa Wazungu mpaka Juma amosi Feb, 9.

Feb. 13, tutawasafirisha mwalimu Leonard Mkwasomba na mkewe, wanaenda kushika kazi ya kufundisha watoto

MSIMULIZI. 738
kule Masasi; na Barnaba Mtaula anapelekwa Masasi kufundisha, na Leslie Namate mtoto wa Newala anarudishwa kule Newala maana ni mdogo na augua marra kwa marra. Mtg.

MBWENI SHAMBA.

Salaam kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Illi wa baada ya hii salaamu, nataraja kukuarifu habari chache za mwaka huu. Kwanza katika Dec. 16, Waliniwasilia watoto watano wanaake wakitoka Mvita, kungojea safari ya kwenda kusayidia Wazungu wao kufundisha watu pande za Mamboya. Ikawa katika Dec. 22, usiku alikuja Mmanga mmoja hana akili kitwani, naye alimfanyia Padre uthia sana, hatta tulimthania ni mwivi tu atoa ujanja, illi aone nafasi ya kuiba; hatta alienenda katika Kanisa la St. Mary akajificha, na kubeba kitabu cha Nyimbo. Wahatimaye, Padre alimpeleka kwa General Mathews, ajue baina. Bali tukajibiwa kama ni mtu aliyepungukiwa akili, tukasikitika kwa kumpeleka kule.

Dec. 17, Mtu mmoja mtumwa atoka pande za Migombani, aitwa Sudi, alikuja kutaka haki, ya kuwa bwanawe humfanyizia shauri kwa siri illi amuuze. Alikuja kwa mashauri kama haya. "Ginsi gani bwana wangu hunifanyia hila, illi aniuze kwa siri! Nami ikiwa kama niwezavyo kutenda, najaribu kumpendeza bwanangu. Hii ndio haki ya miaka hii?"

Naye alipelekwa mjini kwa Balyozi kwa habari hii.

Dec. 24, Mbele ya siku kuu yetu ya Kuzaliwa Bwana, usiku tulifanya Sala kubwa, kwa furaha ya siku kuu. Ilikuwa katika kanisa kubwa, juu yote tulifurahi kupata watu waliopokea misalaba, ndio hawa, Sulemani, Nasoro, Kankanakwa, Selenge, Uledi, Uledi Mbiza; wake Mama Diva, Kangangwa; na watoto wangine wa kike wa nyumbani.

MSIMULIZI. 739

Na siku kuu yenyewe hiyo nakuambia ilivyokuwa shangwi! Wenyi ngoma ya Kinyasa, wenyi ngoma gani, pia mchanganyiko. Wallakini furaha zaidi ya kuwa watu wengi sana walipokea Usharika Mt.

Dec. 22, Perpetua Kamna alijaliwa kupata mtoto, bali mtoto wenyewe aliugua kifua sana, na Mama mtu aliugua, hatima katika Dec 27, Mtoto yule aliitwa, R. I. P. Katika Dec. 28, Siku yao Wasio na hatiya, ndugu yetu Mwalimu Stephen Shanti alikuwa hawezi, huko pande za Uwandani, na Dec. 28, aliitwa na Muungu, kutoka taabuni, R. I. P. Jan. 12, Padre Key alienda Mrima Dare-salama akarejea Jan. 15.

Jan. 4, Watoto wale wa Mvita walienda Mamboya.

Jan. 24, ilikuwa harusi kati ya Uledi Mbiza na Dora Mtendama. Nawaarifu kama sasa nyumba ya Bibi Miss Mills imekaribia kwisha. C. M.

MBWENI.

Salamu sana kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Na baada ya salamu napeleka kwako habari zipitazo hapa petu, nazo ni hizi.

Feb. 2, siku kuu ya Utakaso wake Bikira Maryamu Mbarikiwa twalishinda hapa hapa petu.

Feb. 7, Tulimpokea Bibi M. A, Berkeley akitoka kwao, bila panapo mwezi ule ule, siku ya 18 akaenda kufanya kazi yake Kiungani, huko ndiko anakokaa.

Feb. 12, Walitiwa mikono watoto wetu saba ni hawa. Stella Chatangu, Augusta E. Mkandala, Sophie Milao, Josephine Eva Asha, Beatrice Mswali, Hanriah Kijakazi, Amani Mabruki, na wawili wa Mjini. Feb. 15, Twalimwaga Bibi Ruth Berkeley aendaye kupunga hewa kwao, lakini aenda Misri kwanza mpaka wakati wa baridi uishe pande za kwao, ndiyo afike. Feb. 24, Mattayo Mt. tulishinda hapa petu. March 24, tulitengeneza nyumba yetu na kupamba Makanisa yetu. Hatta March 25, Ee! Furaha, furaha, kwanza kama saa thenashara ilifanyika sala katika Kanisa lake Bikira Maryamu Mbarikiwa, hii sala ilikuwa ya Kiingreza. Hatta saa ya kwanza

tukaenda kwa Kanisa lake Yohana Mt. Hapo ikafanyika sala na shangwi kuu likawapo, wengi wetu wakampokea Mfalme wa Wafalme, hatta waliojitenga kwa siku nyingi wakaonekana. Siku kuu zilizofuata tulishinda hapa petu.

March 31, Tulikaribishwa Kiungani kwa siku kuu, tulifurahi mno, tukashinda kule, jioni tukarejea kwetu. April 2, Tulipata Kuhubiriwa kwake Bikira Mbarikiwa tulishinda petu tukijifurahisha na michezo yetu ya killa siku. April 3, Tulikarimiwa mno na Bibi yetu Miss Thackeray,

MSIMULIZI. 741

alitufanyia karamu kuu, katika shamba lake, tena kombe la wali kweli kweli lilikuwa, kuku na miwa na ndizi. Wote walionekana kufurahi mno sana, karamu hii ilifanyika kwa kusudi la siku ya Kuzaliwa kwake huyu Bibi. K. Sh.

SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, naja kwa machache wala si kwa mengi mwezi huu.

Feb. 2, Alituwasili hapa Timothy Matitu akitoka pande za Uganda, naye alileta habari ya kuwa ndugu mmoja amefariki huko jina lake Ibrahim Mdonde. R. I. P. Katika Feb. 4, Ruth Zariga alipata mtoto, wallakini si rizikiye.

Katika Feb. 12, Bwana Askofu mbele ya kwenda zake pande za Bonde, alitia mikono watoto wanaake watatu, katika Kanisa la Bikira Maryamu, pamoja na watoto wa nyumbani, watoto wa Shamba ndio, Hanna Kijakazi, Amani Mabruki, na Beatrice Tatu. Na katika siku hiyo, hatukusoma kwa siku kuu ya Bwana Askofu. Katika siku hiyo hiyo, usiku wake wa kutazamia Feb. 13, Ndugu yetu Titus Mataula, aliyeugua siku nyingi, aliitwa na Muungu kutoka taabuni za dunia hii, maziko yalikuwa saa edashara. R. I. P.

Feb. 24, Jioni aliwasili Padre Denys na mkewe akitoka pande za Mrima Dare-salama kwa kubadili hewa juu ya ugonjwa wake wa kifua. March 16, Charles W. Rehani na mkewe wamesafiri kwenda Uganda. Katika March 24, mbele ya kutazamia siku yetu ya furaha ndio ya Pasaka, ilikuwa sala kubwa kama ilivyo kawaida mbele ya siku ya furaha, wallakini ilikuwa ndani yake, kubatizwa watoto wangine watano

MSIMULIZI. 742

wa Shamba. Na majina yao ni haya: Diouusio Frederick Ibrahimu, Soter Augustino Ramathani, Stephen Jabu, Onesimo Sefu, Evaresto Kajoka.

Katika siku ya Pasaka tulifurahiwa sana, hatta siku ya Juma a tatu, ilikuwa ngoma ya Kinyasa, naswi hatukusoma Juma nzima, na siku ya Juma amosi March 31, Tulikaribishwa sote Kiungani, hatta jioni tukarejea.

April 2, Padre Denys, alifunga safari ya kurejea kwake na mkewe, pamoja na Alice Faraji.

April 4, Alituwasilia Emma Nasibu kutoka pande za Bonde, akifuatana na Bwana Askofu; bali yeye hajatuwasilia bado huku kwetu. Tena leo leo, walifika hapa watu hawa: Kambenga na Mpambeni wakitoka pande za Uganda. C. M.

MSARAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu, wabaadu ya salamu nakuarifu kama siku nyingi sana hamjasikia habari za kwetu kuweni rathi sana, balli msitumainie kupata habari nyingi, kwani nalikuwa usingizini; bassi yaliyotendeka siyajui, illa niliyofahamu mbele ya kulala ni haya:

Tumefurahi mno kumpata Padre hapa Msaraka kwani zayidi ya miaka 4 hatukuwa na Padre illa huja tu kwa siku yake, kumbe sasa amekuwa hapa daimara.

Mwaka jana ilikuwa matata sana kwa Wabondei, karibu Bonde yote, wamefuata amri ya mwanamke mzee akaaye upande huu, Akasema Kama, Amechukuliwa mbinguni, na ameambiwa kama kunakuja ugonjwa mkubwa sana, utaletwa na watu watakaotumwa, bassi killa

MSIMULIZI. 743

mtu heri wajenge nje ya mji kibanda kidogo; wazike mtoto wa kuku ndani yake: tena watie killa aina ya mbegu juu ya kaburi la kuku waliyemzika kibandani mle. Hivyo watu watakaotumwa mbinguni wakifika nje ya miji ile watapumzika, tena watakula mbegu zilizotiwa, tena marra watasahau kuingia mjini; wataenda zao pasipo kuuthuru mji. Na maneno mengi sana aliyosema, bassi killa upitapo wakati ule waona kibanda nje ya mji. Marra kwa marra anasema maneno mengi, washenzi huamini. Pangine husema leo watu wasitembee, nao wangine wanamsikia illa wangine wanamsema sana hatta husema, Heri afe kuliko kutaabisha watu.

March 10; tulienda Magila kwa kusudi la Padre Peter Limo atapokea daraja ya Ukasisi, akapokea March 11, watu wengi walikuwako. Na ni furaha mno kumpata Kasisi wetu wa inchi hii, zayidi twatumaini Wapelekwa walioletwa Bonde wamepata kujifunua nyuso zao, kupata tunda la inchi bii, ijapo wakiwa wamerudi kwao, illa hawakukaa burre naswi katika inchi yetu.

Katika Juma hizi mbili zilizopita tulipata kukamata nzige wengi wengi, Ah! ajabu hiyo bwana, walifunika kabisa mawingu, na kama sauti ya ngurumo moja kwa moja wakiendea pande za mashariki, siku hizo killa mtoto hatta mzee wamo majanini, wanakamata nzige, hatta nussu walianguka hapa petu tukakamata.

Hatta sasa wanaonekana mmoja mmoja majanini, mashambani pia, mpunga umeharibika mwingi mashambani, ikawapasa kupanda tena, maana hapana dalili ya kuwa palipandwa mpunga.

March 19, alasili tulienda Magila kusudi ya kufanya faragha ya Roho, ilikuwa Juma atatu jioni hatta Juma a tano assubui, killa mtu akarudi kibandani kwake.

Ijumaa Kuu tulikuwa hapa, illa saa kumi tukaenda na Padre Lawson Umba, akashikwa na homa, tukarudi

upesi. Marra tulipofika hapa twawaona wapagazi wa Mr. Cowley wa Msasa wanatua hapa petu, hatta tulipokuwa tukishangaa mwenyewe atokea, alifuatana na Mdachi; walikaribishwa illa maana hapana nafasi, huyu Mdachi alisimika hema hapo kiwanjani petu, na Bwana Cowrley akalala juu. Assubui wakaenda zao, kumbe usiku ule wa Ijuma Kuu mke wa mwalimu wetu alipata mtoto.

Siku kuu ya Pasaka tulienda wote Magila tukarudi Juma a tatu.

March 29, Bwana Askofu alituwasilia hapa akishuka kwenda Unguja pamoja na watoto:

Francis Mzimba na Nataniel Bungulu waenda Kiungani kujifunza. A.J.

KOLOGWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa. Tumeanza kujenga nyumba yetu ya mawe, kiisha kujengwa zitajengwa nyumba zingine tatu; moja ya watoto, ya pili chuo cha kusomea, na ya tatu ndilo Kanisa. Tumefurahi mno kumpata Mwalimu Cleraent Kathibeni anatusayidia sana, bali sasa amerudi Kiungani. Mtoto mmoja amebatizwa siku hizi jina lake Samwili Kiwayo. Labda utanena mbona hupati habari zangu, ah! ni maana shughuli nyingi, tunafundisha watu mjini killa Juma a pili na watu wengi huja kusikiliza maneno ya Muungu. Tena karibu mwezi huu watabatizwa watoto watatu, tena wamefanywa Waanafunzi watu watano: Mahujo, Manyainguli, Mwedadi, Sagaiya na Mbelwa.

Feb. 20, Alikuja hapa Bwana nduguye Padre Chambers kumwamkia, nasi tukafurahi mno kumwona. Lakini alipoenda zake Unguja alitufanyia karamu kubwa alitununulia mbuzi tukamla. Tena alikuja Mwalimu Petro H.

MSIMULIZI. 745

Musa kuja kupunga hewa kwa ugonjwa wa macho, lakini amerejea tena Unguja. Y. Ch.

MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam, wa baada ya salaam, naona mwatuthania tumelegea kuwapasha habari za hapa petu lakini sivyo, najaribu kuwaandikia mimi mwandishi mpya ninayeanza mwaka huu. Tumefurahi ndugu zetu sita wanaake wamepokea misalaba na majina yao ni haya; Mamgwiya, Mamsaka, Mamhando, Mabasuna, Nkauhu, Makiango. Alikuja Mr. Roberts kuja kutazamia watoto kusoma, na katika class ya 1 Cathbert Mlangwa, 2 John D. Sayidi, 2 class 1 Chambingo, 2 Herbert Ngaja; 3 class 1 Lemjenje, 2 James Ungutu. Daktari Ley akaja kututazama akitoka Magila, tena Daktari Ley pamoja na Mr. Roberts wakarudi pamoja. Tumefurahi kumwona mwalimu Edward Kingodi kutoka Unguja aliye hawezi macho aje apate afya ya macho yake. Watoto walipewa ruhusa yao kwenda kwao mda wa juma 2. Mwalimu Archie na mkewe wameenda Unguja ili kusoma, Padre Griffin akaja hapa Mkuzi, siku ya pili akarudi Magila. Mwalimu Willie J. Swedi ameanza kazi ya kufundisha hapa Mkuzi.

Feb. 3, huzuni kuu tuliyo nayo ya mtoto wa mwalimu Henry amefariki R. I. P.

Feb. 19, tulifurahiwa ya watoto wawili Harry Kidungwe na Herbert. P. Mhaka wakitupa habari kama Bwana Askofu kaja amepita njia ya Tanga.

Feb. 3, Padre wetu akaenda kuonana naye, siku hiyo hiyo Dr. Ley kaja kumtazama mtoto aliyebaki wa Henry Nasibu kwani naye hawezi. Feb. 21, Padre Dale arudi.

Feb. 26, tumepata mvua kidogo kwani miezi yote hii mvua hatujapata ilikuwa jua tu, watu sasa waanza kupanda na kulima pia kwani walikuwa wakingoja mvua tu. W.J.S.

MSIMULIZI. 746

MIWA.

Nawaarifu habari zetu chache za hapa, tu hali gani; na tunaendaje kwa hali yetu tuliyonayo.

Lakini la kwanza najua wapo wa'nne watano watasoma habari zetu na jina hilo la Miwa wallakini wasijue ni wapi na mahali gani na watu gani hao? Kama miye zamani naliwaza maswali hayo.

Bassi hapa ni mahali kati ya Chitangali na Newala na Masasi, mwendo wa saa a tatu kwenenda Chitangali, na kama saa a sita mpaka Newala, na saa kumi ao edashara kwenda Masasi.

Na mahali penyewe pamevumbukana kwa kujenga chuo na Padre Cecil l890; Kwanza hakuweza kupata Mwalimu upesi lakini akampeleka mtu mmoja aliyejifunza zamani kusoma Kiungani. Bassi yeye akaanza kuwafundisha watoto. Muda wa siku nyingi kidogo akapatikana Mwalimu kuja kuwafundisha watu wa hapa wazima na watoto — 1891. Yule mwalimu ni Sipriani H. Chitenje, akazidi kutenda kazi hii, hatta watu wazima thenashara na vijana watatu wakaonekana wamestahili kupewa misalaba kuwa waanafunzi, tayari kwa Ubatizo; wakapewa Juma a pili ya Mitende katika Kanisa la Bikira Maryamu Chitangali 1893. Mwalimu huyu amekwenda Kiungani kujifunza zayidi kusudi baadaye arudi hapa, nami nimeshika kazi yake.

Twatumaini watu wale watabatizwa mwaka huu 1894, na wangine twatumaini karibu kuchaguliwa kupewa misalaba kuwa waanafunzi.

Furaha sana kusimulia ya kwamba watu wa hapa wanaendelea sana na wanaonekana wanataka sana hali hii ya kubadili maisha yao ya zamani ya giza na kufuata Umasihiya.

Sasa tuko katika kujenga kanisa letu, watu wa

MSIMULIZI.747

hapa wanajenga burre pasipo gharama ya kutoa Mission; nalo juu limekwisha bado chini tu, na twatumaini kuisha mbele ya Pasaka ao marra Pasaka ikiisha.

Feb. 23, nalikwenenda Chitangali kumwona Padre, masikini watoto wake wote nikawakuta hawawezi ugonjwa uitwao Kiyao "Chikuku," billa wale wawili wakubwa Florence na Mona; na mdogo mwingine alikwenda Newala pamoja na mwalimu Rose. Safari ile ile kabla sijarudi Miwa tukaona msafara wa akina Barnaba wakatupasha habari za jamaa huko Unguja. Tukafarajika. Salamu Y. M.

MASASI.

Wote wasomao Msimulizi huu salaam. Najaribu kuwaarifu kidogo hali yetu sisi Amasasi. Tu wazima kabisa kwa habari hizi. Kweli marra nyingi sana sana hamkusoma nyakati hizi tulizo nazo sasa niandikapo habari zetu, illa mmezisikia tu kwa watu, na kitu cha kusikia hakipatani baba, habari nyingi labuda za kubahatishwa tu, haifai kutucheka tuanzapo habari za zamani za kale. Mlisikia ya kuwa mwalimu mkubwa wa Masasi ndiye Paul Kasese, baada ya kufundisha kwa siku nyingi sana na kuelemisha watoto, kunako mwezi wa September alirejea pande za Unguja kubadili hewa, na mahali pake amekuja aandikaye habari hizi kunako November 3 aliwasili Masasi akitoka huko Unguja.

Kunako Dec. 17, nalikwenda Newala kushariki habari za Retreat, hatta 22 nikarejea hapa.

Dec. 27, & 28 wageni wengi sana watokao Newala, Miwa, Chitangali; kwa nia mbali mbali, wangine kuangalia jamaa zao, na wangine kuangalia Wamasihiya wenzao hapa Masasi tupate kufurahi pamoja. Walikaa

MSIMULIZI. 748

mpaka Dec. 30, wakarudi zao. Jan. 30, mwalimu Luke Chivoko alikuja Masasi. Jan. 1, watoto wa school ndogo ndogo wakaja kunako school yao kubwa udio akaapo huyo awapashaye habari hizi.

Jan. 9, Ilikuwa kutazamia watoto, wallakini sio darasa zote illa darasa ya 1 & 2 tu. Aliyeshinda wa kwanza katika darasa ya kwanza, 1. Michael W. B, 2. David L.L. Katika darasa ya pili 1. Sulemani, 2. Nambasya.

Feb. 23, mwalimu Leonard Mkwasomba alituwasilia akitoka Unguja pamoja na mkewe, nayo siku ile ile tena aliwasili Mr. Cook, akitoka Newala. Tulipata furaha kubwa sana sana, kusikia kama watoto waliotoka pande hizi ndio Benedikto Klementi Njewa na wangineo kama wazima pia. Tena furaha sana kwa ndugu yetu Isaya F. Mwalinjila kaingia Chamani mwa Paolo Mtakatifu, na tena kupata kuwa mwalimu. Natega na kufungua. Kitendawili! Tega. "Mwili wangu mdogo lakini una mafuta." Maana yake "Mwili wangu" ndio habari zangu zimekuwa kidogo tu. "Una mafuta," tia akili utajua maana ya mafuta, mafuta mtu akila pangine kitoweo kinakuwa kizuri sana na kitamu sana sababu nyama yenyewe imenona. Lakini tena mtu akila nyama ilionona, mafuta yake labuda yatamkinaisha upesi pasipo kula sana. Vivyo na habari zangu, pangine zitamfurahisha asomaye na asikiaye, pangine zitamchukiza asomaye na asikiaye, kama mafuta hayana pake.

March 8, kafika Mdachi mmoja alikuwa pande za Nyasa ana watu wapata 10 na Wabondei wamo ndani. Sasa wenzetu siyo kutembea huko, wametia maji kabisa loo! Ilikuwa safari kubwa sana ya Wazungu wapata 10 kuzidi kamwe, pamoja na Bwana mkubwa wa Daresalam nao wamepita ndani kabisa mpaka wafike Kilwa Kivinje &c. naye Mzungu atoka Tanga, kafuatana na wapagazi watokao Tanga. Salaam. K.M.

MSIMULIZI. 749

KICHELWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nitaanza kukuelezea kidogo habari za hapa tangu kuja. Nimefika hapa mwezi wa April 1893 pamoja na Bwana Key; tukaja hatta hapa mahali panapoitwa Kichelwe, kijiji kimoja wanachokaa Wamasihiya wachache waliotoka Mbweni, pamoja na watu wa mipakani pande za Mbweni. Hawa watu wa Mbweni wamejigawanya sehemu mbili, sehemu ya Wayao ndio wakaao Liwalani, na Wanyasa ndio wakaao Kichelwe. Wakame wakaao mbele kidogo ya Kichelwe mwendo wa nussu saa; Wangindo ndio wakaao Mibulani. Kusudi lao wasikilizane wakiwa kabila, na sehemu hizi walivyojigawa wana wakubwa wao.

Kuna wangine tena wakaao Mtoni, mwendo wa saa mbili unusu ao saa tatu itatimia, hawa ndio wamechanganyika, lakini hufunga safari kuja kufundishwa na kusali marra moja kwa juma. Kuna wangine machanganyiko vile vile pande za Semeke, Jang'ombe, mwendo wa saa, nao huja kusali siku kwa siku assubuhi tu.

Safari yetu tulipofika hapa pamoja na Bwana Key, ruksa ya kujenga hapa hatukupata kwa wenyewe Majumbe wa hapa, kwa maana walikithani tutawanyang'anya, wasielewe vema na shughuli tuliojia, kwa miezi miwili unussu wasitukubalishe kujenga hapa, halafu yake kwa shidda walitukaribisha. Nyumba ikasimama; miti ndio ya boma lenyewe, kamba, boriti kubwa kubwa, kujenga, kukandika, na shughuli zote zinazohitajia katika nyumba walifanya wao, tangu waanaume hatta waanawake wa vijiji vyote nilivyotaja hapa walikuwamo katika kusayidia.

Mwezi wa July niliposhuka Unguja naliiacha nyumba bado makuti na kukandikwa, wakaimaliza wenyewe pasipo kusimamiwa. Mwezi wa August niliporudi pamoja na mke wangu nikaikuta milango tu ndio bado.

MSIMULIZI. 750

Tangu kufika hapa watu kuja kufundishwa wamedumu, asiyekuja siku zote hatta kuufikia uwanafunzi amepata alama thelathini, aliyekuja siku zote hatta kuufikia Uwanafunzi amepata alama hamsini kwa miezi tissa. Kufika kwangu hapa nimekuta watu waliowekwa tayari kufundishwa zayidi ya 50 wake na waume, halafu yake wamezidi kuja hatta wamefika 122. Pamoja na Wamasihiya na Waanafunzi, itakuwa jumla ya wote waliomo katika mji Dar-es-salaam wenyewe na huku mashamba 192, na mwezi kwa mwezi huja. Naona katika miezi niliyokaa Dar-es-salaam ndio tangu mwezi wa April 1893 hatta February 1894; bassi killa mwezi huja kuniambia, "Mwalimu, andika jina langu, nataka kufundishwa," wake kwa waume husema hivi, nao kutoka katika vijiji vile vile nilivyovitaja. Na hawa watu asili yao si wote watu wetu wa Mbweni, walio Wamasihiya ndio waliotoka Mbweni na Waanafunzi kupata 10; lakini wote hawa ni watu watokao mipakani ya Mbweni, na wangine ni mahuru wa Mdachi, bassi huja kukaa nasi huko shamba. Katika hawa watu wanawake ndio wengi kupita wanaume, naona mtapenda hatta kusikia kama katika wangine wao wamepata kuozwa kwa harusi ya Kimasihiya, hawa ndio wa kwanza walioozwa katika watu wa hapa kupata watu watatu wameozwa na Mr. Key. Tukikusanyika wote mnamo Juma a pili mahali hapo tunaposalia hapatutoshi, sharti wangine wasimame nje. Katika siku hizi za Kwaresima, wamefundishwa kutoa sadaka walio Waanafunzi na Wamasihiya, walifurahi sana kutoa killa mtu alitoa alivyoweza kwa Juma mbili na Wamasihiya pia wametoa. Tena nathani mnakumbuka yale maneno yanayotakwa sana yaenee katika Upelekwa wetu, ndio watu wajue kuwaruzukia wanaowahubiria Anjili ao kuwafundisha, haya ndio maneno anayowaambia wahudumu wake Baba wa dini, anachukulia mambo ya

MSIMULIZI. 751

zamani Wamasihiya wa kwanza walivyokuwa wakitenda. Paolo katika waraka wake mmoja anaeleza. Bassi mimi nimekaa Dar-es-salam miezi 10 u nuss, na katika miezi hii walivyoonyesha hawa watu kama pao pataka mtu wa kuwafundisha, kwanza wamejenga nyumba, kweli mali nussu ni ya Mission, yametumika katika jengo ndio kuwasayidia juu ya makuti na fito, na kamba za nazi na pao na kombati, nyingi za kukata wenyewe. Tena si hivi tu ninavyotaka kusema, lakini wanaitunza, kutunza kwake wakiiona mahali panavuja wanapanda na kuezeka, ikibomoka mahali wanakandika. Tena mmejua ao mmepata kusikia kama hapa mahali tulipojenga nyumba hatukuwa na ruksa ya kulima, lakini wao ndio waliokuwa wakienda kwa Jumbe wa mahali pale kumwambia wataka mahali tumlimie mwalimu wetu tumpandie mhogo; lakini ilikuwa shidda sana kukubali Jumbe; halafu akatoa ruksa kwa ajili ya kuuthiwa vile marra wamekwenda marra wamekwenda. Halafu akatoa ruksa mlimeni, bassi kulima kwao wamezungusha nyumba, na mahali penyewe tunapokaa sehemu kubwa imenunuliwa na Serkali ya Dachi. Zamani za kwanza watu walimao mpunga walikuwa hawana buddi kutoa kodi, kitwa rupia ao kutoa mpunga wenyewe, lakini sasa sababu limenunuliwa hulima burre. Bassi hawa watu isiwatoshe vile walivyolima karibu na nyumba; bassi wakakusanyikana kupata watu 40, neno lao ni hili: "Tazameni sisi tumelima mhogo na mabawe ya mpunga, tunajua kama tutakapovuna hatuna buddi tutamkumbuka mwalimu, walakini kwa siku ngapi? labda wangine tutachoka, na hapa yapo mashamba mengi ya mpunga tukalime moja ikitokea riziki tutajua isipotoka tutajua: ikitokea riziki majira ya kuvuna tutamvunia, tuseme, Mwalimu wetu hiki ni chakula chako." Wala hili halikuwa shauri langu hatta kidogo, sikuwakusanya kusema nao, nami nikashangaa kuwaangalia tu bassi;

MSIMULIZI. 752

wote watu arobaini na Wamasihiya waliotoka Mbweni wamo wakalima shamba kwa siku mbili, na kuja kupanda vile vile, siku ya tatu wakaja kupanda mbegu za kupanda kama mpunga nimetoa mimi. Wakati wa kufunga (Kwaresima) walipoelezewa kwa siku hizi ndizo siku za kufunga za Kimasihiya, bassi ngoma zilizo kijijini pale, wenyewe wakazileta kwangu ziwekwe. Juzi hapa nilipokuwa nikifunga safari ya kuja huku, Juma a pili nilipokwisha kuwasalisha na kuwahubiria pia, tayari kutoka kwenda zangu, marra nikasikia, "Ngojeni wote kwanza"! wakakaa nje wote, bassi neno nililolisikia ndilo, "Mwalimu anakwenda zake, bassi msithani ya kuwa mwalimu anakwenda zake ndio tusahau Juma a pili, ao mtu asahau aenende akafanye kazi siku ya Juma a pili, yafaa tumkumbuke Muungu katika kazi zetu zote, wala sio akiwapo mwalimu tu ndio tumkumbuke Muungu, zayidi asipokuwapo Mwalimu." Bassi wakatoka, mimi sikumtuma huyu mtu, hasha,! alikuwa kama ameniambia, Mbona hukutuambia maneno tufanyeje ukitoka, kwani nilipokwisha kuwahubiria nikajua kushika njia ya kuja Unguja.

Jan. 12, Mr. Key alifika hapa akawatia Waanafunzi watu wanaume 9, na watoto 2 na wanawake 27.

Jan. 14, walipotiwa, majina yao haya wanaume, Madang'anya, Ambali, Saburi, Alisadala, Mabruki, Feruzi, Kitambi, Chiwaula, Nyama, Hamisi na Jarufu.

Waanawake, Ambali, Salama, Biziki, Nyamizi, Mwipile, Mamamwalimu, Hasina, Mwajuma; Siwema, Maua, Amini, Alima, Mamastala, Fayida, Hamisa, Arusi, Hasina, Alima, Zanabu, Binti Hamisi, Zafarani, Yangumacho, Mwajui, Nawene, Mwanamtiti, Chiletele na Chausiku. D. S.

MSIMULIZI. 753

KIUNGANI.

Salamu wote wanipokeao na kunisoma habari zangu na kuangalia ginsi nilivyo rafiki wa Msimulizi na mwenyi kicheko kwa wote wasiyonitharau mimi Msimulizi.

Baada ya salamu yangu nawaarifu kama Feb. 12, wameingizwa kuwa Waalimu, Leonard M. Kamungo, Francis Sapuli, Isaya F. Mwalinjila na Barnaba Mtaula. Tena siku ile ile Patriki Kiaka na Fabiano Songolo wamepelekwa Mkunazini kwa Mr. Lisjter wapate kujifunza kazi ya maisha yao,

Feb. 13, Bwana Askofu ametia mikono watoto watano ndio, Boniface Toro, John D. Mlangwa, Viotor Magonga, Marko Mradi, na Yustino Dodo.

Feb. 15, Reginald H. Songolo amerudi Unguja akitoka Nyasa pamoja naye watoto watano, Leonard M. Kangati, William B. Mpota, Musa Mnjema, Michael R. Kamaliza na Julius Mkonda.

Naona wengi wenu mnamfahamu yule Bibi aliyekaa Kiungani maisha yake yote alipokuwa hapa Unguja, kwa kutusayidia sisi tunaokaa hapa, na Bibi yule jina lake laitwa Miss J. Bartlett. Bassi alishikwa na ugonjwa sana hatta ni mthaifu sana kwa uzee uliompata, bassi daktari amemwamuru arudi kwao Ulaya Ingereza, bassi ikamlazimu kwenda. Naye hakupenda hatta kidogo kutuacha wala sisi hatukupenda atuache, bassi.

Feb. 17, tulienda wote Mkunazini kumwaga, akaingia ndani ya meli akasafiri.

Feb. 18, Ametuwasilia Bibi mwingine kuja kukaa hapa badala ya yule aliyekwenenda Ulaya Ingereza jina lake Miss M. A. Berkeley, zamani alikuwa akikaa Mbweni, bassi bahati ya mtu haiko mbali, ndiyo tumeruzukiwa aje kukaa hapa. Kweli naye wa kufaa sana na mtendaji kazi vile vile, bali sasa niandikapo barua hii hayupo

MSIMULIZI. 754

yupo Mbweni amekwenda kupata hewa maana atoka pwani, twatumaini atatuasilia baada ya siku si nyingi. Siku ile ile ya Feb. 18, Gray Feruzi amepelekwa Mr. Lister Mkunazini anafanya kazi ya "Gazette."

2, Ametuasilia hapa Mwalimu Denys Sayite na wakitoka pande za Mrima Dares—Salam, alienda Mbweni, na akatuarifu kama Paul Twagonge hawezi.

March 1,

BWANA CHAMBERS alikuwa hawezi sana, hatta alichukuliwa Mkunazini kwa English Hospital, na kule ugonjwa ukamzidi. March 4, Juma a pili, tulipotoka kwa sala ya Eucharisti Takatifu, marra tukaona barua ya kusema anatazamiwa kukata roho, ndio panapo saa pili urobo; tukaingia kanisani kumwombea. Tena penyi saa sita kasorobo ikatuwasilia habari ya kutuarifu kama amekwisha kufariki. Marra tukaingia kanisani kwa sala ya kuombea roho zao waliofariki katika Imani; tena saa saba watoto wote tulienda Mkunazini kumwangalia marra ya mwisho. Ah! kweli ndio huzuni kubwa iliyotuangukia, maana bwana amependa kumtwaa astarehe katika taabu za dunia hii. Ndugu, kweli hatta leo hivi tumetindikiwa mno hapa Kiungani kwa kuondolewa yeye, maana alionekana kuwa mtu wa kufaa sana, mwenyi bidii kwa shughuli zo zote, za chuoni, na za nje pia mamoja kwake; hatta elimu zingine za hapa za chuoni zinasinzia zinataka mtu mwingine aje aziamshe. Bassi tulipokwisha, saa kenda unussu tukachukua mayiti yake tukaja nayo hapa tukaweka kanisani. March 5, assubui tukaenda Ziwani kwa maziko na watu wengi waliokuja mazikoni. R.I.P.

MSIMULIZI. 755

Feb. 28, Mr. Mallender pamoja na Petro H. Musa walisafiri Mrima Dares—Salam kusudi akamlete huyo Paul Twagonge apate kutunzwa na kuangaliwa vizuri. Tena siku ile ya maziko ndipo Bwana Mallender na Petro H. Musa waliporudi hapa wakimleta yule mtoto mgonjwa niliyemnena juu, ah! huneni kama ndiye kwa ginsi alivyokonda, tena kukaa na kusimama hawezi hatta kidogo, bila ajua kulala tu, naye yuko Hospital.

March 6, Ilikuja barua ya Bwana Askofu kunena kama Clement Kathibeni amekwisha kufanywa Msomaji, bassi tulipewa nussu siku ya kucheza.

March 25, Bwana Askofu wa Nyasa amewasili hapa Unguja, kusudi aende zake Ulaya Ingreza maana mgonjwa, alifuatana na mtoto mmoja wa Blantyre. March 18, Juma a pili ya Mitende, amesafiri kwenda zake Ulaya Ingreza akipita njia ya kusini pande za Kepi.

March 22, Tulitenda tayari kazi zote za nyumbani kama tutendavyo Juma amosi.

March 23, Ijuma Kuu, sala zote tumezifanya papa hapa.

March 24, Marra tulipokwisha chakula cha assubui tukaanza kazi yetu ya kupamba nyumba yetu na Kanisa letu pia, bassi jioni ilikuwa sala kubwa sana ya shangwi, kiisha walibatizwa watoto kenda majina yao ndio:

Martini Kaluma, Albano Tambile, Arthur Nyandala, Nikodemo E. Asmani, Yohana Mdala, Timotheo Mabruki, Mikael Masongelana, Petro Chinde, Nikolao A. Salehe.

Ah! furaha mno kuona kundi lote hili kuingizwa katika jama ya Kimasihiya na kuwa waana wa nuru.

March. 25, Siku ya Pasaka, ndio furaha kubwa maana Mola wetu Isa Masiya ndipo aliposhinda kufa na Ahera, bassi saa kwanza ilikuwa Sala kubwa ya dini yetu Wamasiya, na wengi waliokaribia mathbahuni pake.

MSIMULIZI. 756

March 26, Padre Hood, Dakta Palmer, na Mr. King, waliwachukua Chukwani watoto wote wa Kiyao na Mtengenezaji wa Msimulizi pia alienda, bali hatukukaribishwa marra moja maana hatukuchukua khati ya Seyidi. Tukaingia ndani ya banda zuri sana lililozungukwa na miti mizuri ya maua na mikomamanga. Usiku marra tukaona gadi la frasi linakuja, tutazame tunamwona Mwarabu aliye msimamizi mkubwa wa Seyid kule Chukwani, akaleta salamu, kusema, Bwana Seyid na Greneral Mathews wamenituma kusema salamu na baada ya salamu wanauliza je! mmepata killa kitu fathili? waima kama mnahitaji kitu niambieni? ao kesho mkihitajia kitu mtumeni huyu Sajin? Akajibiwa hatuna tulilopungukiwa, kamwambie Bwana ahsante. Marra akaingia gadini akarejea mjini.

March 27, tukafunga safari ya kwenda Haitajwa balli tusifike maana ni mbali yataka saa sita kwenda na kurudi.

March 28, marra ilipopiga saa kumi tukashika njia ya

kurudi hapa, na wangine walio wagonjwa wa miguu waliazimiwa punda, killa mtoto alifurahi sana kule Chukwani. March 29, Meli ya Ulaya imekuja pamoja na Padre Travers aliyetuacha kwa ugonjwa sasa kama miaka kumi, bassi tumefurahi mno kumwona marra ya pili, naye yupo hapa kwa siku hizi chache. Balli halafu ataka azunguke katika miji yote ya Upelekwa wetu mpaka Nyasa, tena akijaliwa arudi kwao Ulaya Ingreza.

March 30, tulitengeneza nyumba yetu kwa kupamba tayari kukaribisha wageni watakaotujia.

March 31, Ilikuwa mkutano hapa, Mbweni na Mkunazini ilikusanyika hapa, na killa mtu alifurahi, na wangine walicheza sana tinge, hatta ilipotimu saa edashara killa mtu akarejea katika masikani yake.

April 2, Siku ya kuishika siku kuu ya Kuhubiriwa Bikira Maryamu Mbarikiwa, tulienda assubui Mkunazini

MSIMULIZI. 757

kwa sala kubwa ya Eukarist takatifu, kiisha tukarudi hapa. Tena siku ile ile tumepata watoto wawili kuja kukaa hapa majina yao, James Kathbeni na Musa Mdekereni.

April 3, ametuasilia Bwana Askofu akitoka Magila pamoja na Mr Henriques na watoto saba wa Kibondei wajao hapa kusudi wachume elimu wakawasayidie nayo ndugu zao.

Na majina yao ni haya: Paul Dezu, John D. Saidi, James Mkumbano, Nataniel Bungulu, Harry Kidungwe, Francis Mzimba, John T. Mbaruku.

Kiungani mwezi huu imejaa sana watoto jumla ni 121 waliopo hapa ndani ya dari hii ya nyumba ya Andrea Mtume.

April 5, Tulicheza siku nzima kwa sababu ya kumfurahia Padre Petro Limo amekwisha pokea daraja ya Ukasisi kule Magila, na tena watoto wanaopiga chapa walipewa siku ile siku kuu maana Agano Jipya limekwisha pigwa chapa, bassi walienda kushinda Mwera.

Tena siku ile ile alituasilia Mr. Kick akitokea pande za Ulaya Ingreza, naye yupo hapa siku hizi. Padre Hood anasafiri Newala na Petro H. Musa na Mr. Mellor anaenda pia. Petro H. Musa ni mgonjwa wa macho, bassi anaenda kwao labuda hewa ya kule itamfaa, apate kurudi tena hapa kujifunza. Mtg.

MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaam. I11 wa baada ya salaam, mtathaa wangu wa safari hii, ah! mdogo sana lakini nitajaribu nikutimilizie mistari mitatu minne, kwani mwenyeji halisi wa shughuli hii amekuwa thaifu hatta hakuweza kukusanya habari nyingi, na nimsayidiaye leo hivi ni mimi Sheldon.

MSIMULIZI. 758

Panapo mwezi Feby 2, mke wa mwalimu wetu W. E. Wasiwasi akapata watoto wawili pacha mmoja maji kunde na mmoja mwekundu, nao wote ni wanaake.

Siku ya 10 pametuasilia bwana W. King akitoka pande za Hindi kupumzika, sasa hajambo na afya zake, naye yupo hapa Mkunazini, afanya kazi yake hapo. Mwezi ule ule siku ya 15 mail ya Kape iliwasili, ikatuwasilishia salama bwana Kerr, atokaye Nyasa pamoja na Reginald H. Songolo aliyekuwa mwalimu kule, na watoto watano wa Nyasa wajao Kiungani kupata ilimu zayidi.

Panapo siku ya 17 mwezi ule Bwana Askofu wetu kasafiri akienenda Magila, katika mail hiyo hiyo wakajipakiza bibi J. Bartlett, bibi B. Berkeley wakienenda pande za Europa pamoja na bwana Kerr pia.

Siku ya 18 mwezi ule ule, watoto wale 2 wa mwalimu W. E. Wasiwasi walibatizwa usiku kama kawaida, yule wa kwanza jina lake Maryamu Konstansi Rehema, na yule wa pili jina lake Edith Harriett Madan, watoto wa Kinyasa & wangine walikuja kuangalia ubatizo.

Mwezi ule ule Feby. siku ya 22, mji wote wa Unguja ulibadilika, sababu? utauliza labda, Sababu ni hii wajua kana tangu kufa Sayidi Ali hatta leo hivi ni zayidi ya mwaka mzima, bassi siku hiyo iliamriwa mji wote upambwe kwa bandera na majani na kwa killa neno la pambo kana hali ya mapambo mliyoyazoa kuyaona. Bassi kwa siku tatu, kwani pambo lilianza nyuma ya 22, bassi mji ulijaa mapambo, pote pazuri na pa kupendeza sana. Wafungwa wakafunguliwa kwa desturi ya kumiliki mfalme, pasipo athabu iwayo yo yote, hatta wangine hawakuweza kujimudu kwa ginsi ya gereza lilivyowazoea. Hatta siku ya 23, ah! baba, uwandani kwa Bwana hakupitiki baba, kwa umati wa watu; watu wamejaa kufanya

MSIMULIZI. 759

nini? utauliza, ah! baba, leo siku ya furaha kwa Unguja yote. Wamejaa kutazama Seyidi Thuwein akipewa milki yake na nguvu zake na uwezo wake, kwa imara ya Waingreza. Askari wa Kiingreza pamoja na Blue Jackets ndio baharia wakashuka uwandani kwa Seyidi, uwanda ukafunikwa na umati wa watu. Viti vya thahabu ao vilivyopakwa thahabu vikawekwa mlangoni katika nyumba ile ya zamani ya Seyidi (sio Bet-el-ajabu) mlangoni safu safu; cha Seyidi katikati na mbele ya viti mimbara mbili zenyi pembe za fetha na thahabu, chini ya daraja la mwisho haya bassi, tuangalie nini? Tazama! tazama! rafiki, nini kile king'aacho? Ah! uzuri mkumbuu wa thahabu bwana, mrefu mzuri, wang'aa. Wa nani ndugu? anavikwa bwana Seyidi. Nani yule amvikaye? Liwali wa kwanza wa Unguja yote, bwana General Mathews na Balyozi mkubwa wa siku hizi jina lake Mr. Rennell Rodd. Nani wale waliokaa pande pande? Nao pia ni mabalyozi. Pana balyozi wa Amerika, wa Italia, wa Wareno, wa Wafaransa, wa Wajermani. Na wangine wale nani? Pana mkuu wa Mabaniani, Wahindi, Waswahili, Waarabu, Wangazija, Waparisi, wa Waajemi, killa mtu kwa ukuu wake na mahali pake, wamevaa uswafi wa mavazi yao na uwezo wao waliopewa. Nini kile? Ah! ndio tepe (medals). Apewa nani? Seyidi mwenyewe. Angalia sana — tazama kilemba kizuri, joho zuri, upanga thahabu, jamvi, mkumbuu thahabu, killa vazi zuri; Ah! fahari gani hii leo? Kweli enzi, mpya killa kitu kimebadilika. Sikiliza! nini? Ah! mjomba, mdundo huo wa Kiingreza. Ah! mbona mzuri? Kweli kwani ni wa kushangilia ati, baada ya yote mizinga ikapigwa, tena kimya, Nini? Mwingreza akapanda mimbarani akanena maneno ya kumheshimu na kumsifu mfalme. Akapanda mkuu mwingine, akanena, tena mwingine, hatta killa mkuu wa killa kabila akaisha. Ah! maneno

MSIMULIZI. 760

yaliyonenwa siku hiyo ni mengi, siwezi kuyanena ndugu, hatta mnamo saa sita ndio baraza ikaanza kuvunjika, killa mtu aenda hemani kwake. Je! ndio bassi? Njoo saa saba utaona yatakayoendelea. Nini? Wangazija bwana, wakaranda kikwao huko Ngazija kana vile Mafiti na Wangoni wakati wa vita na baragumu lao wakipiga kwenda kwa vita, mwenyi mkuki ndiye, mwenyi bunduki ndiye, mwenyi upanga ndiye, Ah! baba, killa ghasia ya selaha, na nyuso zimepakwa masizi na rangi, illi kusudi viogofye. Ah! mambo haya leo, Unguja ni Ulaya ni Shenzini, mambo hayo yakaisha kwa mchana mmoja tu, zawadi zilitoka kwa Bwana, ndio marubabi wakapewa wale wachezaji, askari wafanyiwa mtee chelo punga,

Ukija uwandani kwa Seyidi utaona nyumba ile ya katikati imeongezwa kwa mbele kana futi tatu na nguzo nzuri za chuma, madirisha mazuri, juu dari vingine imejengwa. Haya, tazama kwa pwani utaona kivuli kimejengwa juu kwa juu cha mabati, chini ukuta imara mnene wa kushindana na mawimbi, na ngazi za chuma za kushukia majini; vizuri pamejengwa. Unguja yazidi killa mwezi, kwa nyumba, watu, na vitu pia, ndio habari.

Panapo Feby 25, katuwasilia Mwalimu Denys S, akitoka Dar-es-Salama, mgonjwa wa kifua, ni tangu zamani, lakini kwa leo hivi kilimzidia mno ndio maana kaja anga aonane na Daktari.

Habari zingine ndio mnamo March siku ya awali, bwana Seyidi alipenda kujaribu kuzunguka Unguja hii kwa merikebu yake, akaendelea vema toka hapa hatta huko juu, marra ghafula merikebu nzima yote ikapanda juu ya jabali moja baharini; Ah! ghafula bwana yote upande. Lakini kwa Rehema za Muungu ikatelemkia majini ikakaa sawa vile vile, Ah! bwana maisha ndogo yalikuwa;

MSIMULIZI. 761

bassi bwana alipoona hivyo akamwambia Nahotha, Ah! bassi sitaki kwendelea mbele tena nishushe papa hapa Mkokotoni. Akashuka akaja zake peke yake illa na watu wawili watatu tu kana mtu fullani naye kwa miguu mpaka Chukwani.

Fikiri mtu mzima toka Mkokotoni hatta Chukwani, kule Chukwani akapeleka simu mjini ya kuwa leteni magadi & wafuasi illi kumtwaa wamlete mjini, yale magadi yakaenenda & askari pia, ajabu hiyo mtu aliyekwenda kwa jahazi sasa anarudi kwa magadi; bassi akaja zake mjini yupo yu hayi hatta leo hivi.

Siku iliofuata, bibi yetu Miss Boyd ameona vema kutazamia akili za watoto wa chuo chetu cha Mkunazini, bassi, Examination ilianza March 6, ikaja zake March 9 siku hizi mbili, maana March 7 ni siku ya Perpetua Mt.; bassi ikawa holela, kwani mtu wa Afrika yule. Panapo March 15 mail ya pande za Kepi ikawasili ikituletea Askofu wa pande za Nyasa, ndiyo Askofu Hornby akitumaini kumkuta Askofu wa pande hizi, illi wapeane mashauri, lakini hakujaliwa kumkuta kwani alikuwa pande za Bonde.

Bassi akawa hana buddi kwenda zake vile vile chini, illi apite pande za Kepi, kwani mizigo yake aliacha huko. Naye yuenenda Ulaya Ingreza kupunga hewa kwani amekuwa mgonjwa marra kwa marra.

Siku iliofuata Charles W. Rehani kasafiri yee na mkewe katika safari ya Bwana Martin kwenda kwake Uganda kwa njia ya Mombasa kwani ndiko kwenyi njia ya Uganda siku hizi.

Siku ya Ijuma Kuu katuasilia mtunza hazina wetu, bwana F. Davenport, akitoka huko & huko tu, kupunga hewa baada ya ugonjwa wake; ah! kule kutembea

MSIMULIZI. 762

baharini kulimfaa sana sana, kwani alikuja mwenyi maungo yake.

March 25, Pasaka, ah! tulikuwa hapa hapa tukajifurahisha tu, kana tuwezavyo, neno moja mtapenda kujua, ndio tumepata Cope mzuri sana sana, imetolewa na Padre Acland Hood kwa sadaka ya Christ church, ah! baba, nzuri sana, kweli, yafunga kwa mbele kwa thahabu & vito, heri ujionee la kuambiana siyo la kuona.

Siku ya Juma atatu watoto wa Sagara ndio watoto wa kazi wa bwana H. Lister walikwenenda Chapwani na watoto wa darasa ya kwanza &c. walikwenda Chapwani pia pamoja na Mr J. Grindrod walikaa upande mmoja wa kisiwa. Nia yao ilikawa kwenda Bawe lakini hawakupata ruksa, kwani siku hizi visiwa vina amri baba, sharti kwa ruksa ndipo uenende kisiwani. Wote wakacheza illa yule paa.

Siku ya 29 mail ya Ulaya iliwasili ikituwasilishia Padre D. Travers, yee amekuja kuangalia Mission zote zi pande hizi, na baadaye arejee Ulaya & kuwapasha habari za kazi ya huku wale wafanyao kazi ya huku kazi ya Mission hii yetu.

Siku iliofuata ndio ya 30, "Marks," za Examination zikasomwa chuoni na Padre wetu Dr. E. Palmer, na thawabu zikatolewa pia, katika darasa ya kwanza wa 1. James Kathibeni, wa 2. Yakobo Matozwe, wa 3. George Uledi.

Katika darasa ya pili wa 1. George Wm. Biu, wa 2. Richard Matimla, & wa 3. Obedi Farijallah. Katika darasa ya tatu wa I. Keto Stanley Mahangu, wa 2. Harry Mgumba, wa 3. Patrik, katika darasa ya nne waj. Jude Ashdon Faraji, wa 2. Andrea Shabani, wa 3. Stefano Taji. Katika darasa ya tano wa 1. Leonardo Faraji, wa 2. Karlo Sudi, & Kathbert Juma, hawa chanjari,

MSIMULIZI. 763

katika darasa ya sita wa 1. Mikael Nasibu, wa 2. Dustani Songolo, & katika darasa ya saba wa 1. Moses. Hivi ndivyo ilivyokwendea Examination yetu, sasa darasa zimekuwa tano tu, kwani watoto wengi wamepelekwa Kiungani kupata elimu zayidi kule. Siku iliofuata ulikuwa mkutano Kiungani, kwa furaha ya kawaida.

Mwezi huu April nimepata barua ya Uganda yatoka kwa Henry Wright Duta, hamna habari nyingi, illa anena wale maadui wetu, tumewashinda, hatta siku hizi amani inazidi lakini bado sana kwani ugomvi hapo na hapo. Tena wengi waongoka kwa dini ya Kimasihiya wakiacha ile ya Kiislamu, tena Waislamu wamepewa mahali pao pa peke yao mbali sana na wao, kusudi wasitufanyie uthia tena ndio habari.

Panapo April 1 katuwasilia bwana Kick akitoka Ulaya Ingereza, pamoja naye bwana Mellor na mwingine sahibuye Mr. Grindrod.

Siku ya 2 yake siku kuu ya B. M. Mbarikiwa sala yetu ilistawi watoto wa Kiungani na watoto wa kazi wa Mbweni walikuja kuabudu hapa ah! baba, sala ya siku hiyo shangwi kweli kweli - njoo uone. Siku hiyo hiyo mwalimu Denys alisafiri zake Dar-es-alaam yee na mkewe na mke wa Nicholas Faraji — aendaye kumtazama mumewe kwani afanya kazi barra hiyo.

Panapo siku ya 3 ya mwezi huo April katuasilia Askofu wetu akitoka pande za Shambara - Magila, kaja na watoto saba wajao kusoma kule Kiungani.

Siku ya April 8, Tumeangukiwa & huzuni ndio mtoto mmoja wa Mr. Lister, jina lake Selywin Ukolo amefariki ugonjwa ulimshika tangu siku ya mkutano, tulienenda kumzika siku ya Juma a tatu. R.I.P.

Panapo siku ya 12, wameng'oa nanga Padre Acland Hood & Bwana Mellor, Mr. Henrigues, na watoto, Petro Musa & Luka Lichinga wakienenda Mgao Lindi. K.W.E.

HABARI ZA KUFARIKI BABA ASKOFU WETU.

May 10, Tulipata habari za huzuni sana kwa simu iliyotoka Aden, kama Bwana Askofu wetu amefariki baharini, kati ya Unguja na

Aden, bassi akazikwa na jamaa yake Padre Travers baharini. Ah! Maskini sisi tumekuwa hatuna jemadari wa Kanisa letu la mashariki ya Afrika.

May 11, Ilikuwa sala kubwa ya Eukaristi katika Christ Church kwa ajili ya roho ya Askofu wetu aliyefariki. Ee Bwana umpe raha ya milele. Alifariki May 7.

Kweli twamshukuru sana Muungu ya kuwa alituchagulia Askofu huyu, ya kuwa alikuwa mtu wa kulifaa sana Kanisa hili, hodari kwa kwenda safari kwa miji ya Upelekwa wake. Aliye na namna njema kwa wote walio chini yake. Tena alionekana kuwa kama mzee sana, kumbe ni mtu mzima tu wa miaka 49, na aliamriwa Uaskofu 1883, amefanya kazi yake kwa miaka kumi. Alikuwa mtu mtawa sana. Twakumbuka kama Wayonani waliopanda waabudu Yerusalemi, bassi hawa wakamjia Filipo wa Betsaida wa Galilaya, wakamuliza, wakinena, Bwana, Twataka kumwona Isa. Yuaja Filipo, amwambia Andrea; yuaja Andrea na Filipo, wamwambia Isa. Jamani sisi tulio watu wa Afrika ndio wale waliokuja kusema, twataka kumwona Isa, na huyu marehemu Askofu wetu hakukataa hatta kidogo, kutoka kwake Ulaya Ingreza, kuja huku Afrika, aliposikia moyoni mwake sauti kubwa ya kunena, Bwana, twataka kumwona Isa ginsi alivyo mwema, ginsi alivyo mwenyi huruma na sikitiko nyingi, asiyependa wenyi thambi

MSIMULIZI. 765

wafe, illa waokoke wapate kuishi. Bassi kwa utawa wake wa bidii aliyotenda ameleta wengi kumwona Isa. Twakumbuka sana mahubiri yake ya mwisho kwetu sisi alituambia, Waanangu wapenzi katika Masiya, angalieni sana, mtakapoendelea sana kusoma elimu ya kweli ya Muungu mtaona vitabu vingi vingine vyenyi maneno ya upotevu sana, yenyi ueresi mwingi ndani yao. Lakini nawaonya sana, kama mkitaka kujua wapi itakapoonekana kweli ya Muungu, ni pahali pamoja tu ndio Msahafu Mtakatifu (Bible). Tena angalieni msitende mambo yenu kusudi mpate kusifiwa nao walio juu yenu, illa kutenda yote kwa sifa za Mola wetu na Muungu wetu.

Tena kazi ingine ya mwisho hapa, ndio alitufurahisha mno kabisa, tukimwona yeye aliye Baba yetu, akija Class Room kuwafundisha waalimu, Ah! ndio fundisho kubwa kwetu. Kweli alionekana kuwa jemadari mwenyi ujasiri mwingi, aliyepigana sana kwa ajili ya Kanisa letu la Mashariki, hatta alionekana thaifu sana, mwenyi alama za mapigano ya jemadari mshujaa, hatta alishikwa na ugonjwa na kufariki. Shindano lililo zuri ameshindana, mwendo wake ameumaliza, imani ameilinda; baadaye amewekewa taji ya haki. Muungu amependa kumtwaa astarehe katika taabu za ulimwengu huu, na mwili wake umewekwa ustarehe katika vilindi vikuu vya Okeani la Hindi. Bwana aliyetoa, Bwana aliyeondoa, Jina la Bwana libarikiwe. R. I. P.

MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaam. Illi wa baada ya salaam haja yako ya killa mwezi ni hiyo nakuletea. Kwanza naona utanirathia sana, kwani nalisahau kutia habari moja, panapo mwezi ule waliokwisha pita March 24, huku kwetu kumebatizwa

MSIMULIZI. 766

wanaake wawili wakaao katika shamba la bwana Muxworthy; majina yao Maryamu na Anna. Panapo siku ya 25 Apr. Watoto wadogo wa chuoni wa hapa walienenda kushinda Sebuleni, pamoja na bibi Boyd na mabwana pia.

Siku hiyo hiyo, hapo Mnazi mmoja kwenyi "Kantiin" kulikuwa thawabu mwajua kama Unguja pana vyuo vingi, bassi pana chuo kimoja kikubwa sana cha Kihindi, ndani yake husoma Wahindi na Banyiani. Na elimu iliomo ndio kujielemisha Kiingreza, Kiguzurati, Koran na mangineyo, jina la chuo hicho huitwa chuo cha Euan-Smith Madressa. Bassi walifanya Exam: mwezi uliopita, bassi hawakupata nafasi kupewa zawadi siku zile, illa siku hiyo Exam: iliisha kabisa, lakini walijifunza Poetry, na wangine kipande kizima cha Somo. Kazi hii ni kwa wale waliopasi waliojulika watapata thawabu, bassi ilikuwa hivi. "Kantiin" ilijaa fuchi Wahindi, Wazungu, Bahora &c. Balyozi mkubwa akaja na mkewe, Nahotha wa H.M.S. Philomel akaja na wangine wawili watatu walio wakubwa pia wakastarehe vitini. Wakasalamiwa na wote.

Baada ya hayo, kazi ikaanza, ndio wale waliojifunza Poetry &c., waliletwa zamu kwa zamu kusema mbele ya Balyozi na watu wangine wawili waliojifunza Maongezi yale yalioandikwa katika "English Fourth Reader" page 129. Ianzayo

H. Have you done what I told you?

G. Not yet Sir.

Na zinginezo zile zile msomazo katika vyuo vingine, bassi wenyi mashahiri wakinena & wenyi maongezi wakaongea, yote yakafanyika kwa Kiingreza; mangine Kihindi, mangine Kiarabu. Baada ya hiyo ndipo thawabu

MSIMULIZI. 767

zikatolewa, sio ngwenjo, la, illa vitabu vizuri, wangine kimoja, wangine viwili, &c., killa mtu kwa kupasi kwake. Hayo ndivyo yaliokuwa siku hiyo.

Panapo April 30 tumepata huzuni sana, ndio mtoto mmoja jina lake Lawrence Mtumwa, yee alikuwa mzalia wa Mbweni, babake ni Rikardo. R.I.P.

Siku kuu ya Kupaa ilipotuasilia tena, hatukujaliwa kwenenda popote.

Panapo May 4, ndipo marehemu Askofu alipong'oa nanga kwenenda Ulaya Ingreza, yee na bwana D. Travers & bibi mmoja wa Hospitali, jina lake Miss A. Brewerton naye mgonjwa.

Panapo May 8, tulipata siku kuu, badala ya siku ya Filipo na Yakobo kwani hatukucheza sababu ni siku ya kufunga. Bassi tukaiweka, mpaka panapo siku hiyo ya May nane. Tupate kujifurahisha nayo, tulienenda shinda miembeni kule Mbweni, karibu & nyumba ya bibi Mills; mnamo alasiri kasiri tukajirudia zetu kwetu mjini.

Panapo May 10, Ah, assubuhi kama saa tatu tulipata simu ya mji Aden, ya kutuarifu kana Askofu wetu Charles Alan Smythies amefariki dunia, Ah, huzuni gani hiyo jamaa, mtaa ukatulia kitambo uliposikia kengele ya huzuni ikilia. Kweli huzuni sana kupata habari kama hizi.

Mnamo siku hiyo hiyo usiku wake, wamesafiri bwana 0. Kick na Petro Sulemani wa Kiungani, na mwalimu mdogo Sheldon aendaye kumwangalia Mwalimu Denys Dar-es-salama; yule Petro Sulemani na Mr. C. Kick waenenda Mgao Lindi, hatta barra Newala.

Siku kuu ya Pentekote hatukuenenda pahali.

Panapo May 15, mke wa Yakobo Chorola amepata

MSIMULIZI. 768

mtoto mwanamke.

Panapo Siku ya sabatashara, Hospital wameletwa watoto wawili wakitoka kwa General Matthews wamekamatwa baharini nao wote wanaake. Wapatapo afya naona wataenenda Mbweni.

Panapo May 24, ukitazama utaona pana siku kuu mbili, moja ya Kanisa ndio Siku kuu ya Eukaristi na ya pili ndio siku ya kuzaliwa Queen Victoria. Bassi bwana siku hiyo wache iwe na mdundo wake. Sikia, kae kitako illi nikueleze habari, baba.

(1) Siku hiyo iliathimiwa iwe siku ya kwata Mnazi mmoja, lakini mvua ilituzuwia kwata haikuwapo, lakini kitu cha pili sikia.

(2) Tangu saa pili hatta karibu saa 4 mvua si nyingi sana manyunyo tu ya marashi.

Bassi Seyid aliitwa kwa Balyozi illi aende kumwamkia kwa ajili ya kuzaliwa mfalme wake Bassi baba, Eh, askari Marinz, walipangwa kwa balyozi toka mlangoni pake hatta mlango wa balyozi Marikani na toka hapo hawa wa General Hatch, na wake yeye mpaka mlangoni pa bwana Seyidi sooo, huku & huku bassi. Yee akashuka huko juu amejivalia joho lake & utemsi pindoni wafuasi huku & huku akapita hatta kwa balyozi, huku mdundo wa Magoa unakula tu. Eh! bwana wacha maneno si nene dunia hadaa baba, hatta ukishughulika kuangalia tu, utachelewa baba. Bassi akafika huko.

Akaamkiana naye yapata nussu saa tu; marra akashuka zake akaingia ndani ya gadi lake, kwani wingu la mvua lilikuwapo, akarejea zake kwake. Bassi huku nyuma wache mdundo ule, miziriga manuarini pia haya tu, holela; mzalia hafi na maji.

MSIMULIZI. 769

Bassi hayo ndiyo yaliotendeka kwa muda huo wa assubui siku hiyo livu tu, hatta hamali hakushusha makanda, Office zikafungwa siku ya kumfurahia Queen Victoria, kwani ni mwaka wake wa hamsi wa usabaini sasa naye yumo tu. Bassi wale wa rayia yake hawana buddi kufurahi kwani wako chini ya amani tangu miaka mingi.

Panapo siku ya 26 mwezi ule ule, mashindano Mnazi mmoja yote hayo ni kufurahia siku kuu ile ile. Mashindano killa namna, kupiga mbio, kupiga mbio kwa kuzunguka, kuruka miti, kuvutana kwa kamba, kutupa risasi la chuma, kushindana kwa punda, ah, baba, killa namna ya machezo uliotokea hapo ulikuwa na thawabu yake, wangine hupokea mende, wangine vyombo vya shaba ao fetha, killa mtu kwa kadiri alivyoshindana. Mashindano yalianza saa nane unussu hatta saa thenashara unussu, zayidi pia. Mnazi mmoja ulijaa umati wa watu, Eh, kwambia Matumbuizo ya mdundo wa Kigoa kati kati bwana, watu wakishindana huku mdundo unakula tu, saa hizo hapana kuchoka tena kwani mdundo upo ati, hema zalitandwa, hatta wajomba wa Mbweni wakaja pia, illi kushuhudu mashindano.

Mnamo saa ya jioni ndipo killa mtu alishika njia ya maskani yake. Aliyepata kwenda kwake na kicheko, asiyepata, Ah! ni hivyo tu, baba, wajua wewe tena hayo.

May 27, Juma a pili kwetu hapa Mkunazini, pamebatizwa mtoto wa Yakobo Chorola panapo saa ya jioni, jina lake huyo mtoto ni Christabel Jane. Ndugu wote wa upelekwa wetu mliopo popote naona mtapenda kusikia habari hizi, ndio panapo May 25, ametuasilia mwalimu John Baptist Mdoe pamoja na mkewe na mtoto wao mdogo wakitoka pande za Magila, na

MSIMULIZI. 770
habari aliyoleta ndiyo yeye baada ya miezi hii mitano amejiwa na fikara ya kuturejea tena kazi ya upelekwa wetu. Bassi yupo hapa Unguja atatwaa mahala pa William E. Kanyopolea, kwani yee aenenda pande za Nyasa tena kufanya kazi yake huko kama kwanza. Ukuta mmoja wa nyumba ya Mkunazini ukatika kuanguka.

NANYANGA.

Salamu kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Wabaadu. Nakuarifu hali yangu ya kuwa njema sana, na mbaya. Kwanza hasema njema ndio ya kuwa sisi tu wazima; sana wote. Na mbaya ndio kama mwaka huu tumepatwa na misiba miwili na iliyo mikubwa sana, wa kwanza ndio tangu kuandama mfungo mosi, kama siku ya thenashara hatta leo mfungo pili tumepata mvua, lakini mfungo wote mvua hapana wala tone moja. Bassi nafaka ya mpunga imeunguzwa yote na jua wala hatuna tumaini nayo tena. Na leo 3 ya mwezi May mvua imeshuka ya nguvu sana, bassi tukitumainicho ndicho mtama huo tunatumaini kama tutakuwa wazima tutaweza kula.

April 20, Ndio msiba wa pili kwa mashamba ya jamaa zetu wakaao nasi wamekuja mapanzi na vyakula vyao vimeliwa vyote toka shina hatta nchani. Bassi wakaenda zao, bassi ukaja msafara wa nyama, huu zayidi kuliko ule wa kwanza, kama wa kwanza walibakiza chakula wao wakamaliza kabisa. Bass twamshukuru sana Muungu ya kuwa jambo hilo baya halikuingia kwetu. May 3, jioni waliwasili watu wawili ndio Andrea Kapanda na Tomaso na mizigo yao ya Padre Acland Hood, wao peke yao, bassi wakatupa na barua za Unguja, mwenyewe akawasili Juma amosi. Bassi nikawa mtu wa kupumzika, maana nalikuwa mtu

MSIMULIZI. 757

wa kwenda Newala kwa Juma pili; bassi tukawa watu kumfanyia tayari yeye. Lakini tukamtazamia Juma a mosi wala hakuja na Juma a pili pia wala hakuja. May 7, katuwasilia Padre Acland Hood, tukafurahi sana kumwona tena akija mwenyi afya, kwani Muungu amependa kumrudisha kwa inchi yetu tena, Juma a tano May 9 akaenda zake Newala akipitia njia ya kwa Akumkanga akaapo mwalimu Pilipo.

May 11, Tumefunga safari yetu ya kwenda Newala pamoja na mke wangu, na tukalala njiani kwani siku hizi njia ni yenyi shidda kwa magugu.

May 12, Tukawasili Newala. Ndizo habari. Salaam. B. Y. M.

HABARI ZA MIWA.

Katika Msimulizi uliopita naliwaarifu ni habari zetu chache za hapa ginsi tulivyopata kuwa katika hali hii tuliyonayo ya kukaa hapa tukifundisha na tunavyoendelea.

Siku hizi tulishika kazi yetu ya kujenga kanisa letu kama nilivyowaarifu katika Msimulizi uliopita. Bassi kazi yetu ya kujenga hilo kanisa ikamalizika Juma a nne; siku mbele ya Siku kuu ya Marko Mwanjilisti April 24.

Ap: 25, nalipeleka waanafunzi wa hapa kutwaa mathbahu Chitangali kwa kanisa letu, kwani huko Chitangali sasa wamepata mathbahu ngine mpya na nzuri sana, bassi ile iliyokuwa zamani Chitangali ni hii iliyoletwa hapa.

Ap: 26, Padre Cecil akawasili hapa pamoja na mwalimu Petro H. Musa toka Chitangali.

Ap: 28, Juma a mosi kanisa letu likatabarukiwa, watu wengi walikuja. Saa ya kwanza ukawa Usharika Mtakatifu, baada ya kutabarukiwa, na baada ya kutoka Sala ya Usharika Mtakatifu ikapigwa kengele ya mahubiri,

MSIMULIZI. 772

wote wakaingia kanisani; Padre Cecil akawahubiria ginsi ilivyowapasa kuheshimu kanisa kwa kuwa imetolewa na kuhesabiwa kuwa nyumba ya Muungu, na pia ginsi ilivyowapesa kulifayidia kanisa kwa sadaka zao.

Siku ile ile Ap: 28, Padre akaondoka kwenda zake Chitangali.

Bassi siku hii ndio ya kwanza Usharika Mt kufanywa Miwa. Watu wa hapa wadumu hatta sasa, wangine wanaongezeka.

Kanisa hili la Miwa limekwitwa kanisa la Marko Mtakatifu kwa ukumbusho wa siku kuu yake iliopita siku mbili kabla ya kutabaruku kanisa hili.

Salamu. Y.M.

HABARI ZA KIUNGANI.

Salaamu kwa wote walio rafiki zangu mimi Msimulizi. Baada ya salaamu, naja tena mwezi huu kuongea tena nanyi kwa machache tu. Habari zangu ndizo kama Apr. 19, tulikwenda kisiwa Chupwani, tulikwenda kwa ukarimu wa Bwana Travers, alitoa gharama kununua vyakula, na akanauli mashua za kutupakia kwenda kisiwani, tusiwe na habari wenyewe, illa tulistukia tu kama tunaenda kushinda mahali. Lakini siku hiyo mvua nyingi ilikunya, tena bahari ilichafuka sana kwa upepo mwingi mno, tukajifurahisha kule kama tulivyoweza, jioni tukajirudia zetu.

Apr. 25, Siku kuu ya Marko Mwanjilisti, alituasilia Mwalimu Clementi Kathbeni, akitoka Kologwe, baada ya kufundisha kule kwa miezi minane. Apr. 30, Tulipata faragha watu wa chama cha Paolo Mt. na waalimu wote wa hapa, tukaenda kanisani saa nne kwani Padre Travers alitaka kutuaga kwa kutupa maonyo juu ya kazi hii yetu ya Ualimu. Akatwaa maneno katika

MSIMULIZI. 773

Yoeli 28, Akatuambia kwa maneno mengi ginsi itupasavyo kumtegemea Muungu, tusikate tamaa katika kazi hii, na ginsi Afrika ilivyo kubwa, nayo kuhitaji yatuhitaji sisi tuisayidie, na kwa maneno mengi akatuonya, na kutupa shauri. Na hii ndio aliyotamani sana moyoni mwake kusema naswi mbele ya kwenda kwao.

May 3, Siku ya Kupaa hatukwenda mahali, illa watoto wa kazi, walikwenda Bububu pamoja na Bwana Mallender na Brough, na wakati wa kurudi walisumbuka sana na bahari, hatta wakarudi saa nne usiku. Na siku hii tulikuwa na furaha sana, kwani chama chetu kinaendelea, kwani siku ille aliongezeka mmoja ndiye Lenard M. Kamungo.

May 4, Bwana Askofu pamoja na Mr. Travers walisafiri kwenda kwao, Bwana Askofu kusudi apate afya, na Mr. Travers alikuwa dhaifu sana. May 5, alituasilia Padre Du-Boulay akitoka Membei, alikwenda pata afya kwani siku nyingi aliugua; naye anakwenda Bonde.

May 8, Hatukusoma tulipewa kucheza mahali pa May 1 kwani tulisoma, kwa kuwa zilikuwa siku za kuombea.

May 12. Walisafiri Mr Kick. na Petro Sulemani kwenda pande za Lindi, Mr. Kick aenda kuanzisha kupiga chapa Newala, na P. Sulemani aenda kaa Chitangali kumsayidia Arthur Kasembe kufundisha.

May 12, Tulimsafirisha Yohana Hamisi kwenda Bonde kutembea kwa siku chache, alifuatana na Padre Key, na siku hii hii, jioni yake walibatizwa watoto sita; majina yao Mikael Pasumba, Yakobo Kalinde, Andrea Landungusi, Filipo Mbulia, Mikael Faraji na Isaya Boli.

May 14, Ndio Juma atatu baada ya Pentekote

hatukwenda mahali, billa watoto wa kazi walikwenda kushinda Sebuleni pamoja na Mr. Mallender.

May 15, Juma a nne baada ya Pentekote watoto nussu walikwenda Sebuleni pamoja na Bwana Du-Bonlay, na watoto wangine walikwenda kushinda Ziwani, tunapocheza mpila.

May 24, Alituasilia Padre Simpson, pamoja na Paolo Kazinde aliyekwenda kutazama jamaa zake, na Saburi, Mikael Maleso, Yusuf Chimbindu, Petru Malesho, Daudi Tovi, Andrea Msuweta, Samuel Msieri, na mtoto mmoja wa Chitangali John B. Nasor.

May 26, Yalikuwa mashindano Mnazi moja ya killa namna, mbio, kuvutana kamba, kuruka, miguu, mitatu, &c. na waliokuwa wakishindana ni watu killa namna Wazungu, Magoa, Wahindi, watu weusi pia, hatta na sisi tulikaribishwa kwa mashindano mawili ya kupiga mbio, na walioshinda vizuri ni Alfred Mpetula, Y. Kolumba Msigala, Fredrick Makuela. Salaam.

MSALAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salaamu, wa baada nakuarifu habari zetu hapa ni thaifu sana; Kwani Padre wetu Lawson kwa siku hizi hana afya sana marra kwa marra huugua, ikampasa kwenda mahali kubadili hewa; hivyo April 12, akaenda Magila.

April 14, Akaja Padre Petro kufanya Missa Takatifu.

April 15, Padre Petro akaenda zake kwa Kibai, ndio jioni ya Juma a pili. Safari ile nathani nimewaarifu habari ya nzige waliopita juu hewani wakifunika mbingu pia, wakiendea pande za mashariki. Kumbe kule wamezaa nyikani, ndio nyika kati ya Bonde na pwani. Bassi wakapanda tena wale watoto wao, Ah! Bwana wee; wakatenda kazi nyika yote majani yasionekane. Ndipo zikaja

MSIMULIZI. 751

mashambani, na sasa ni wakati wa mihindi na mtama kumea, ikawa killa shamba waingialo ikitimu saa ya kwanza unussu huoni hatta dalili ya kuwa shamba hili lilipandwa kitu. Bassi ikawa kazi ni hiyo, hatta kunako siku ya Jumaa tatu April 16, saa saba twaona umati wa nzige, babu wee ginsi walivyoshikana havineneki, wanawasili hapa, sauti moja kwa moja hwa-a-a-a-a-a-a mithili ya mtu atiaye muhindi uliopukuswa katika kanda ukitoka kaponi. Mashauri? hatuna, tukishangaa vile marra nyumba imepambwa (maana hawa hawajaruka wanatambaa tu,) nikafunga madirisha. Wapi baba, walijipenyesha matunduni wakajaa chekwaa ndani killa pahala. Nje, Ah! hakukanyagiki, walituuthi mudda wa siku tatu, illa nje wakawa wakipita usiku na mchana zayidi ya Juma a tatu. Bassi je! watu wa Msalaka na mji wa Mkumbi na mji wa Jaila (ndio, vijiji vilivyozunguka station hii) wamekuaje? Hutwaa fagio wakifagia juu ya nyumba, illi manyasi ya nyumba yasiliwe. Wakawa katika ukali huu muda wa Juma moja na zaidi, watu hawawezi kuzungumza usiku nje illa kwa shidda. Kumbe mwisho wake inchi nzima ikawa njaa ndio mwisho wake.

April 22, Akaja Padre Petro kufanya Missa Takatifu, kwani Padre wetu hajapata nguvu.

April 29, Akaja tena Padre Petro kusudi lake ndio kufanya Missa Takatifu akatuarifu kama Padre Lawson hawezi sana kule Magila.

May 2, tukaenda Magila kwa siku kuu ya Kupaa, nikarudi siku ile ya Kupaa jioni peke yangu, nikalala kwa Mwalimu Lewis Bondo.

May 7, wakawasili Padre Lawson akichukuliwa wavuni pamoja na Mr. Roberts na mtoto wa chuoni cha Magila Sekiubi, tayari kushuka pwani ya Tanga. Padre Lawson akiwa ameshikika sana ikampasa kwenda

MSIMULIZI. 776

Ulaya Ingreza na Bwana Roberts akimtunza hatta afike katika meli.

May 11, Tukasikia kufa kwa Bwana Askofu ndio siku nikaenda Magila kwa siku kuu ya Pentekote. May 14, tukarudi pamoja na bibi yangu kwani tangu Kupaa hakurudi sababu ya mto wa Magila ulijaa, na siku hiyo tu ilikuwa kwa nasibu nikapata Wazigua wakamvusha yeye na mtoto. Ah! watu hodari sana kwa kazi hiyo nikawapa ujira wao, siye wenyewe tukaogolea. Marra tulipofika hapa hatujapumzika sana tukamwona mgeni Wetu aliyefurahisha watu wa hapa ndiye Padre J. K. Key akifuatana na Mr. Roberts na mgeni mngine ndiye Mwal. Yohana Hamisi wakija kutembea, na Mr. Roberts akarudi Tanga kwa kumtunza Padre Lawson. May 15, Mr. Roberts na Yohana Hamisi na wapagazi wakaenda Magila.

Padre Key akaenda Mkuzi, akajitembeza katika viambo hivi Umba, Kwe Rusanga, Kiole, Kwa Mkuna, Kwe Mkonga, Zingo, tena Mkuzi kwa siku hiyo moja ndio viambo vyenyi marafiki wake wa zamani. Sasa watu wanaanza kupanda tena mahindi illa zaidi choloko na mihogo na namna ya maboga, maana upande huu wetu nzige zimetoka kabisa, illa wale watoto moja moja nao wanaruka, ndio heri kidogo kuliko wakitambaa.

May 25, Padre Key amefika hapa assubui akikusudia kwenda Unguja Juma atatu, atakaa nasi siku tatu; siku ile ile akaenda Mlembule alasili kutembea, akarudi jioni. Usiku kama saa pili tukaenda naye Padre kuhubiri katika miji ile mitatu iliyozunguka hapa petu, tukarudi nyumbani saa tano.

April 26, akaenda Umba kwa Juma apili, Mwalimu

akafuata assubui yake kama saa edashara unussu. Akarudi athuuri pamoja naye.

Usiku wa Juma apili kama saa pili tulipokuwa tayari kutoka kuenenda mjini kuhubiri kwake kwa mwisho, marra twawaona watu wanatua mizigo barazani, tulipouliza habari kumbe ni watu wa Bwana H. W. Cowley wa Msasa, marra twamwona mwenyewe pia anakwenda Tanga kupata afya maana hawezi ndio siku ya 27 ya April. Watakwenda kesho. Wapagazi wake nussu ndio wale watu wa Sangapo ao Singapore wasemavyo wenyewe. A.J.

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Baada ya salaamu napeleka habari zetu kwako, nazo haba tu. Panapo siku kuu ya Marko Mwanjilisti, hatukwenda popote tulishinda hapa petu. Tena kwenyi siku kuu yao Filipo na Yakobo Mitume tulishinda hapa petu tena.

May 3, Kupaa, sala ilifanyika kama Juma a pili. Pentekote 13, wengi wetu walioenda kumpokea Mfalme wa wafalme, Juma a tatu tulishinda hapa hapa, Juma a nne pia hatukwenda pahali.

May 9, tulipata siku kuu kwa Padre Peter Limo wote tulifurahi sana mno, waungwana wetu waliona vema tuende sebuleni, bassi tukaenda kushinda huko hatta mnamo jioni tukajirudia kwetu.

May 12, Padre wetu bwana Key alikwenda pande za Bonde kutembea kwa siku chache, na May 29 alirudi, tumefurahi kumwona. May 24, Wametufikia mwalimu Rose na watoto watatu wa Padre Cicel wajao kusoma, naswi twaliwapokea kwa furaha, kwani twaliwatazamia sana. K. Sh.

MSIMULIZI. 778

MAOMBOLEZO JUU YA ASKOFU SMYTHIES.

Piga kengele ya huzuni kwa mshujaa, Kwani mshujaa hapana tena; Amezama amefunikwa chini ya wimbi, Kwa kassi na haraka karibu na bahari ya kwake.

Enyi Afrikana wa upande wa mashariki! Amkeni! Sikieni! kengele ya thahiri, Yaliaje hiyo? ngoo! ngoo! moja, moja! ni mlio wa huzuni! Nani ameanguka leo? habari zatoka wapi?

Zatoka kaskazini kuvumako pepo za mja naswi, Zatokea juu kwa simu ya mji Aden; Zatokea baharini zivumako pepo na wimbi likarusha, Je! simu yasemaje? funua haraka tusomee yote.

Ah! ndugu enyi weusi mlioteuliwa, Baba yenu mkuu na Askofu ameanguka, Bado siku tatu kufika mji Aden; Muungu amependa kumchukua.

Ni yupi mmoja wapo? kwani wamesafiri wawili, Naye wa pili atosha kuitwa baba? Ah! kweli wee mwenyi maarifa ya kuuliza sana, Lakini wanijua — aliye wako hassa.

Ni yee Askofu wako, Charles Alan jina lake, Yee uliyemzoea kumwangalia mikono na uso wake; Yee aliyekaa nawe kwa miaka kumi hassa, Ndiye, Ndiye, aliyeanguka leo.

Bassi je! wee Afrikana hulii? Kwani umenyang'anywa baba na mchunga wako.

Nilieni? kwani aliyenipa ndiye aliyenichukulia, Kamwekea mahali pema penyi hewa ing'aayo.

Huzuni moyoni imejaa, Laiti ningeona uso ao mkono wake: Sikitiko na kilio zimenifumba, Laiti ningechukua kaburini maiti na jeneza lake.

MSIMULIZI. 779

Lakini yee aliyetuumba alipenda yote yawe yaliotokea, Yee aliyetoa yee aliyeondoa Jina la Bwana lisifiwe; Juu lipewe heshima na sifa, Chini litukuzwe likaogopwe.

Yee aliyetupa alipenda awekwe katika vilindi vya maji, Yee aliyetutolea kwa furaha na shangwi hakuhitaji amweke mbele yetu; Illa amependa kumtenda mbali naswi, Si kwa shangwi si kwa Nyimbo illa kimya kalala kaburini.

Enyi maji vilindi na bahari, Enyi Nyangumi na viumbe vikubwa; Enyi nyote mliomo wadogo kwa wakubwa, Pokeeni wekeni vema sanduku hilo kwani umo mwili wa msafiri.

Bassi sasa nyote mliopo nyama wa majini, Na nyie viumbe vya juu; Huzunikeni, lieni, sikitikeni: Kwani Afrikana hawana bwana tena kwa muda kitambo.

Lakini je? yasiwe hivyo? kwani ndio lazima, Leo upo kesho haupo wanyauka kama jani kondeni; Hayana buddi kuwa kwani ndio alivyoandikiwa ajaliye, Shariti apokewe afukiwe na viumbe za majini.

Bahari ndio sanduku lake, Vilindi ndio kaburi lake, Uronda na dagaa ndio udongo wake; Na vyote viliomo ndio mashitiri yake.

Bassi enyi Afrikana kengele ya Mashujaa, Yalia kwa huzuni na furaha; Mashujaa hapana tena, Wote wamelala chini ya jua. Sasa sharti iwe sifa, heshima, Ukuu enzi na utukufu, Yee aliyetoa yee aliyeondoa; Jina la Bwana libarikiwe, likasifiwe. W.E.K.

KIUNGANI.

Jamani, mimi Msimulizi naja kwenu kwa wakubwa na wadogo pia, maana mimi ni mtu wa maongezi tena nimetaramu wala si mjinga. Balli uwongo tuache na tunene kweli, mtu akinena, waweza kuishi billa chakula usimsadiki. Nami nina wafuasi wengi katika pande zote za Upelekwa huu wa Universities Central Afrika, nami wameniahidia watanilisha kwa habari zao killa mwezi wa pili; bali naona wawili ao watatu tu wanaonilisha, wala sishibi kama miaka ya kwanza. Sijui kwa nini? Hivyo nyie waletaji habari mnathani mimi sasa ni Goboleni? Hasha, mimi ni mzalia wa Seneda.

Bassi kaeni kitako niwahadithieni kisa changu. June 1, Padre Key amerudi Unguja pamoja na Yohana Hamisi wakitoka pande za Bonde.

June 5, Zilikuwapo harusi nne Mbweni, kati ya Hugh S. Mtoka na Christobel Majulia, Clement Kathibeni na Victoria Siila, Danieli Abdallah na Mary Selina Namsisili, Stefano Rehani na Nina Mwayeva. Bassi vijana nussu vya hapa na nussu vya Mkunazini, walikaribishwa kwa karamu ya harusini. Hatta zilipotimia saa kumi unussu, akina bwana harusi wakatawanyika killa mmoja katika masikani yake, machezo mengi yalikuwapo, Mnyasa siku hiyo alichaga kwa ngoma, na Myao ngoma yake, na Mzalia wa Unguja akacheza ngoma yake dandaro na kiumbizi.

July 9, Herbeti Sehiza amesafiri kwenda Mkuzi kuwatazama jamaa zake, twatumaini atarudi tena hapa.

MSIMULIZI. 781

July saba u ishirini, Padre Peter Limo kawasili hapa akitoka Mrima Pangani, amekuja peke yake ndani ya meli ya Kidachi; naye amekuja kusudi aoe, bassi harusi yake itakuwa August 21.

Siku hizi tumekuwa watu wa mang'amung'am tu juu ya kuja kwake Askofu wa Mvita, maana tunamtazamia sana.

July 30, Assubui mapema Askofu aliwasili Mvita akitoka Ulaya Ingreza, bassi panapo saa pili kassorobo akapeleka simu hapa Unguja, ikamwasilia Archdeacon wetu saa pili unussu. Wajua ulimwengu siku hizi umetaramu mno kwa ilimu dunia, hiyo simu ikatwaa dakika hamse wa arobaini tu kufika Unguja toka Mvita. Hii Simu ilinenaje? Mimi naona heri nije meli ya mwezi wa August, lakini nyie mwaonaje? Akajibiwa, Lazima aje, maana killa jawabu aitiwalo lipo tayari. Bassi ilipomfikia akaanza kufunga mizigo yake, marra hiyo aona meli hiyo-o-o inakwenda zake Zenjibar. Bassi siku ile ile alasiri akaleta Simu ingine kunena, Meli imeniacha, akaarifiwa Adimeli, akapeleka simu kwa H. M. S. Thrush impakie upesi, maana H. M. S. Thrush ilikuwa Mvita, bassi ikampakia. August 1, Saa nane hatukusoma, tuliambiwa kama Adimeli atakuja hapa Kiungani acheze kwata. Bassi saa kumi watoto wa Mbweni walikuja pamoja na mabibi yao kusudi waangalie kwata. Saa kumi urobo tunaona askari Marinz hawa wanakuja na selaha zao, wakaja zao mpaka mlango mkubwa, bassi wakapangwa safu kwa safu pande za kuelekea pwani. Bassi hawa Marinz ngome yao ilikuwa nyumba ya Kiungani na Karantin. Marra hiyo tukaziona mashua za Adimeli thenashara zinakuja, mashua za moshi nne, na killa moja yao imefungasa mashua tatu; bassi zikaja mpaka hapa Kiungani, zikatweka bandera ya kuuliza, vita ao amani?

MSIMULIZI. 782

Marra huku pwani zikawaka marra mbili, Mwanamaji naye akapiga mizinga ya mashuani, hatta kufumba na kufumbua waana maji wamekwisha kushuka pwani. Bassi Marinz zikawaka, na baharia naye zikawaka, tena Marinz wakakimbia; mpaka njia kuu, wakapitia kisima cha Baniani, tena wakawasili ngome yao ya pili ndio Karantin. Lakini wapi baba, naye baharia yu macho, walipoitwaa nyumba ya Kiungani, wakapiga, Hip! Hip! Hip! Hurrah. Tena wakawafuata Marinz, na bunduki zikawaka mpaka Kikwajuni, marra baharia wakaizunguka Karantin pande zote. Tena baharia wakapiga ukelele mkubwa mno, Hurrah! Hurrah! Hurrah! Marinz na baharia wote wakaachiwa ruhusa wakaingia Karantin kupumzika. Walipokwisha pumzika, wakasimama safu kwa safu, ukapigwa mdundo wa Kiingreza, bassi waana maji wakarudi zao merikebuni. Na umati wa watu waliokuja kutazama ni mwingi, tena killa mtu akarejea katika masikani yake.

Aug, 2, Saa kumi tuliambiwa kama tunatakiwa kwa mashindano ya mpila, tushindane na Wazungu wa Admeli, bassi saa kumi urobo tulienda ziwani tukajiweka tayari. Haya mashindano yakaanza tukacheza wee-e-e balli si kwa nguvu mno, tukawafunga mabao matano kwa billa mwanda wao. Kiisha tukajirudia zetu hapa, ndipo tukapata baina ya kuwa Alhamisi ijayo yatakuwapo mashindano mengine lakini yasitokee hatta leo hivi.

Tena nimesahau habari moja kama Nikolao Mehege amesafiri Uganda mwezi wa July katika safari ya Mr. Muxworthy. Siku ile August 2, alituasilia Askofu wa Mombasa tulifurahi kumwona, Usiku wa siku ile ikaanza (Retreat) Faragha ya rohoni kwa ajili ya Yohana B. Abdallah & Mr. Radford mpaka August 4 Juma a mosi assubui. Bassi habari kubwa mno iliyotendeka siku ile August

MSIMULIZI. 783

4, labda wangine wenu mtauliza, jambo gani hilo? Sikiliza bassi, Saa kwanza assubui kengele zikapigwa, marra wageni wengi wakaja weupe na weusi. Kanisa likajaa watu. Ikaanza Sala ya taratibu ya kuamuru Mashemasi baadaye likatokea jambo la furaha mno ndio kumwona ndugu yetu mmoja Yohana B. Abdallah akiamriwa daraja takatifu ya Ushemasi pamoja na Mr. Radford, bassi jamani si furaha hiyo? Muungu ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Isa Masiya, azidi kupokea sala ile inenayo: Ee Bwana mkuu wa mavuno ya ulimwengu, mbegu zile zinazomea sasa zisinyauke wala kupobea kwa uvivu wetu. Uwamiminie ndugu zetu Wamasihiya Roho yako atakasaye, na neema yako juu ya makafiri waongoke. Uondekeshe, twakusihi, Wangoje watakatifu katika watu weusi.

Aug. 5, Assubui Juma apili tuliona jambo kubwa, na tulisikia jambo kubwa, katika vinwa na mikono ya wangoje watakatifu weusi. Bwana wetu alisema kwa faragha na wanafunzi wake, "Heri macho yayaonayo myaonayo ninyi, kwani nawaambia, Manabii wengi na wafalme walitaka kuyaona mtazamayo ninyi, wasiyaone, na kuyasikia msikiayo wasiyasikie."

Bassi Padre Peter Limo akatoa Eukaristi takatifu, na Yohana B. Abdallah akamsayidia, ni mbaraka mkubwa tulishwe chakula cha roho na ndugu zetu weusi. Tena panapo sala ya assubuhi saa nne, mwalimu Archie A. Semanyi alifanywa Msomaji, hii ndio furaha ingine. Siku ileile Juma a pili usiku saa kwanza unussu tulienda mjini kumsindikiza mwalimu Yohana B. Abdallah maana anakwenda Unangu kufundisha kule, lakini atapita kutazama jamaa zake kwanza Chitangali. Amefuatana pamoja na Archdeacon Jones-Bateman aendaye Newala kupunga hewa kadri ya miezi miwili atarejea tena hapa. Lakini pamoja na Archdeacon, wamesafiri

MSIMULIZI. 784

watoto watano waendao Chitangali kuwatazama jamaa zao kwa mweusi mmoja kiisha watarudi. Majina yao ndio, Francis Sapuli, Gilbert Y. Mpalila, Alfred Mpetula, Augustine Malemla, na Ambrosio Mitande. Tunafurahi juu ya Gilbert Y. Mpalila kwa sababu amefanywa Mwalimu, bassi safari hii amepelekwa akaanze kazi ya kufundisha pande za Mwiti.

August 6, Tulienda tusali Christ Church assubuhi, na watoto wengi walitiwa mikono, hapa walitiwa mikono watoto kumi na sita ndio hawa James Kathibeni, Martini Kalunia, Albano Tambile, Greorge Asmani, Arthur Nyandala, Nikodemo F. Asmani, Yohanna Mdala, Timotheo Mabruki, Mikael Masongelana, Petro Chinde; Nikolao A. Salehe, Yakobo Kalinde, Andrea Landungusi, Filipo Mbulia, Mikael Faraji na Isaya Boli, kiisha sala tukarudi zetu. Tangu August 6 hatta 8 hatukusoma.

August 12, Imewasili safari va Uganda, bassi tumefurahi kumwona Yohana Sonjo aliyesafiri kwa Siku nyingi. Salaam. Mtg.

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu.

Baada ya salaamu, panapo June 5, palikuwa harusi nne kati ya Hugh S. Mtoka na Christabel Majulia, Clement Kathibeni na Victoria Siila, Daniel Abhallah na Mary Selina Namsisili, tena Stefano Rehani na Nina Mwayeva.

June 11, siku kuu ya Barnaba Mt., hatukwenda popote, twalikaa hapa petu. June 24, Yohana Mbatizaji, hatukufanya Masomo yetu ya killa Juma a pili. Kwani kama tujuavyo ilikuwa Juma a pili.

June 29, Petro Mtume, twalishinda hapa hapa.

July 2, lilikuwa kusanyiko la chama cha Watakatifu

wote, siku ile ile Mathbahu yetu ikazinduliwa, nayo ya Mawe, ni zawadi tuliopewa na Marehemu baba Askofu, kwa Kanisa letu jipya la Mary Mt. Mbarikiwa. Hatta panapo alasiri akaja Archdeacon kuwahubiria watu wa chama. Wakafanyiwa karamu.

July 9, kusanyiko la chama cha Mchungaji Mwema, Rev. Key akahutubu, panapo saa nhe ilikuwa chai katika shamba la Bibi mwalimu. Tena Aug. 9, assubui tulitoka hapa, tukaenda kushinda kisiwa Chipwani chenyi makaburi ya Wazungu, mvua ilikuja kidogo tu manyunyo, na ilikuwa mawimbi sana. Tulifurahi sana hatta jioni tukarudi zetu hapa. Salaamu K. Sh.

KILIMANI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, wa baada nakuandikia habari kidogo za hapa mahali petu. Mahali gani hapa Kilimani? Hapa Kilimani ni pande zizi hizi za Mbweni; kama umejua kule miembeni, kwenyi visima vingi, ndio karibu yake hapa, bali sisi tumekaa kwa juu, karibu na pwani. Ulipata kusikia kama katika msimulizi mmoja kama Bibi Mills aliomba ruhusa kwa marhemu Baba Askofu, ya kuwa ataka jenga nyumba pande hizi za Mbweni, kwani mwaka jana alipokaa huku Mbweni kwa mwezi, pamoja na watoto wake, aliona kama kuliwafaa sana, na hewa ya hapa iliwakalia uzuri. Bassi ile ruhusa akapewa, nyumba imejengwa, nayo si kubwa, kadri tu. Imejengwa vizuri sana, boriti ni vyuma vitupu. Nyumba yenyewe ina vyumba vitano, viwili vya watoto, viwili vya hawa Mabibi, Bibi Mills na Bibi Clutterbuck (Huyu ni bibi anayemsayidia kutunza watoto alikuja mwezi wa May 30 pamoja naye Bibi Mills, alipotoka kwao Ingreza safari hii,) na chumba kimoja ni cha wageni. Tena na baraza mbili, moja juu na moja chini. Mahali hapa pazuri sana, hewa, tena

MSIMULIZI. 786

upepo mzuri, kivuli tele cha miembe, hapana makelele mengi kwani tumejitenga, tuko peke yetu. Mahali pazuri sana.

Watoto wanaokaa hapa 42 pamoja na mwalimu Sheldon, na Jiles Kushelwa, ni mtumishi wa nyumbani humu, na Benedict Madalito yupo hapa kwa mwezi. Tena mpishi anayepika ni Mackenzie Maweyawa na Fabiano Mzee, wamepika tangu June 21 hatta July 19, kwa siku hizi mpishi ni Yakobo Chorola. Tena Miss Whitbread amekuwapo kwa siku chache, kupumzika kwani nyumba ya wagonjwa (Hospital) wagonjwa wazungu hawamo. Watoto walihama wote nusu June 22, na June 25 wakaja wote. Na desturi yetu ndio watoto walio waimbaji (Choir) killa Juma a mosi huenda kulala Mkunazini tayari kuimba Juma pili. Kwani tangu walipokuwapo ni Choir wa Christ Church, bassi nalo ni Cathedral, haliwezi kukaa Juma apili pasipo waimbaji wake.

Kusali tunasali Kanisa la Yohana Mt. hili la huku Mbweni Shamba. Siku hizi tumetengeneza kiwanja cha kucheza mpila watoto, karibu tutakiisha, nacho kiko karibu sana na pwani. Na nyumba tangu kuhamia, wageni wengi wanaokuja hapa kumtazama. Bibi na nyumba pia.

July 19, Baliozi mkubwa alikuja hapa kumtazama Bibi. Tutazidi kadri tuwezavyo kuleta habari zetu za hapa. Mwezi huu August bibi Miss Mills alikuwa hawezi sana homa na kifua, amepelekwa Hospital, lakini leo hivi niandikapo hajambo kidogo tu.

Tena mtoto mmoja jina lake Ayub amefariki, siku ya pili akazikwa. R. I. P., Salamu.

MSIMULIZI. 787

MASASI.

Salaam. Baada ya salaam, ndugu zangu, yanipasa kuwaambieni habari zetu za siku nyingi, Bass sisi sote watu wote amani si amani kabisa kwa siku hizi chache. June 6, waliwasili Manjorinjori watatu walipelekwa na Bwana mkubwa wa Lindi kwa shughuli zao za inchi. Bass ndugu zangu nakuambieni mfano, "Majogoo yakiwika, mwana Adam aanza kuamka, na ndege zote zafurahi pia che! che! che! &c. Sababu wanafurahi kuona mchana tena. Bass maana zake ndio haya. Mwezi June unapokuja, macho yangu na ya wengine yainuliwa kutazama njia za pwani. Bass panapo June 18, tunaona safari inakuja ya Lindi; bass tukatoka zetu tuangalie safari. Bass ghafula tulikuwa na furaha sana sana kwa sababu ndugu zetu Mwalimu Isaya, Klement B. N., Gayo S., Yona M., Cecil M., Patriki K. walituasilia wakitoka pande za Unguja kuja watuangalie, nasi tuwaangalie.

June 19, tulipata siku ya kucheza kwa sababu ya ndugu yetu Rev. P. Limo.

June 28, watoto wa chuo cha Masasi wamepewa ruhusa ya kwenda zao wasayidie mama zao kuvuna chakula.

June 29, Mimi na Clement Njewa tulikwenda Nairombo kutembea tu. Mwendo kama wa saa sita toka hapa. Tukarudi. K. M.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji Salamu sana, wa baada, leo nimenia kutia mkono kukuarifu hali zetu, kwani kwa siku nyingi hujapata taarifa yangu. June, Mwezi thenashara, Aliondoka hapa Mr. Cook kusafiri kwao Ulaya pamoja na Mr. Kick aliyekuja hapa

MSIMULIZI. 788

kusudi afanye kazi ya kupiga Chapa, lakini alizidi kuwa thaifu hatta asiweze kukaa sana akarejea Unguja.

June, mwezi 18, Ikawasili safari ya pwani pamoja na watoto wanne watokao Kiungani kusoma, na Padre Grinrod. June, mwezi 22, Tulipatwa na msiba, ndio ndugu yetu Rikardo Sulemani akafariki, R. I. P. Tukaenda mazikoni siku hiyo hiyo ya Ijuma alasiri, kwani alifariki majira ya adhuuri. Ndiye Mwalimu aliyekuwa anafundisha Makonga kwa Akundonde. Badala ya Mr. Cook tumepata Mwalimu mgine kutusayidia hapa, ndiye Petro Sulemani.

Mwezi uliopita tukapata habari kwamba Lindi wameshuka Sombe (nzige) wanateketeza tangu chakula hatta majani. Marra hiyo tukasikia wamepita karibu na Mikindani, tena tukasikia wameshuka mpaka Mtamba. Sisi tukatumaini kama tumeokoka, kumbe juzi juzi hapa akaja mtu kutuarifu kama wale Sombe wapo Nakalala, tukamwuliza jinsi gani? Akanona wamerudi mapindi huko pande za Mtamba, wakikwea kuja juu ya Rovuma, hatta watu wakilia, kwani mtama haujakatwa. Mwenyi Matola akatuma watu kwenda kuleta ashuhudie, wakaleta tele, shahidi macho yangu. Napo Nakalala na hapa si kitambo kikubwa, kama mwendo wa saa a tatu tu, lakini hapa hawakufika, keshoye tukasikia kama wapo Mchaulu, na huko kuna mashamba ya watu wa hapa. Lakini hao Sombe hawakula, wanatua tu juu ya mtama, lakini hawali sijui kwani mgumu. Wakakaa huko kama siku mbili wakatoka.

July, mwezi pili, Padre Hainsworth na Padre Hood walisafiri Mkoo, kwenda kutazama mawe ya chokaa, kwani waliitaka hiyo chokaa. Lakini hawakuyaona, kwani kiongozi wao alipotea njia, wakashinda siku moja wakaja zao.

MSIMULIZI. 789

Siku hizi nne tano zilizopita kulikuwa na mgogoro wa vita vya Makwangwara, dunia yote ya Newala ikihangaika, kwani walipata baina kwamba Makwangwara wanakuja lakini waendako hawajulikani. Bassi kwa killa mtu akijihadhari mjini pake, kwa mda kidogo tukapata kusikia kwamba habari zote ni uwongo hapana vita.

Kumbe leo hivi July 9, Tunapata habari kama wale Makwangwara wameingia kwa Mangoni wanapigana. Na Mangoni hao ni wa ng'ambo hii ya Rovuma, nao ni jirani sana na sisi, Ng'ambo ya pili ya Rovuma amepita Mboani na jeshi lake, na upande huu ni Chipolopolo. Sijui kama watakutana mbele tena. Hiyo ndio taarifu nikuleteayo kwa mkono wangu. Salaam. S. Ch.

LIKOMA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu, wa baada ya salaamu nakuarifu habari kidogo, ndizo hizi. Labuda ulisikia kama Austini alitoka hapa Jan. 23, kwenda Msumba, kumsayidia mwalimu A. Ambali. Tena ulisikia Akuizombe kupigana na wale Wangoni iliingia njaa kwake. Bassi marra kwa marra watu wa Akuizombe walikuwa wakija hapa Msumba, Pachiya, Chisanga kununua chakula. Panapo Feb. 28, walitoka kwenda Kukobwe, kwani waliitwa na mfalme Mataka, kwani kati ya Akuizombe na Mataka ni rafiki. Bassi walipokuwa wakirejea njiani wakakutana nao wenyi ngao, nao ulikuwa usiku, marra Wangoni wakawaona Wangulu wakawakamata watano, huyu wa tano alikuwa mtoto. Myao akaipiga bunduki, Mgoni chini mkavu, ngao kaichukua zamani gani, imetatuliwa vipande vipande bwana. Wangoni walipoona vimoto, baba wote mguu niponye.

Juma amosi ilikuwa baraza kwa mfalme Masumba

MSIMULIZI. 790

na Masanche, kwani Wayao walitaka kwenda Chisanga kupigana nao, lakini hawa wafalme wakawazuia wakawaambia wangoje kwanza, bassi wakawasubiri, kwani Wangoni walisema watawarudisha. Wakatazamia wee wala hawakuwarudisha. Je! alifanyaje Mwana wa kiyao? alikuwa rathi kwa hayo? Hakuwa rathi bwana, alikuwa na ghathabu kana mbwa mwenyi wazimu, walitoka hapa wengi na bunduki zao kwenda Chisanga. Walakini walipofika Pachia walisikia kama Masawa yupo, naye Masawa alivalia vitu vyake vya vita, lakini yote hayo yalikuwa ya burre majisifu si kitu. Marra alitokea Myao mmoja na bunduki yake mkononi anaranda nayo, alipoona Masawa akaenda kwenyi matete akajificha. Mfalme Maendaenda akawazuia asiuawe, kwa bahati Masawa aliokoka kanwani mwa simba. Hatta hivyo walitaka wavunje Ohisanga, lakini wametulia siku hizi kwani wapo wenyi nguvu zayidi ya wao. March 23, twalikusanyika Msumba Wamasihiya wa Pachiya na Chisanga, walikuja hapa. Hatukwenda Likoma kwa sababu pande hizi Wamasihiya wamezidi kuwa wengi, bassi ndio maana hatukwenda. Apr. 7 Walitoka Msumba kuja hapa Likoma. Apr. 15, wanawake 38 walifanywa Waanafunzi, wanawake wa chuoni Baba ndio hawa: Wonife, Peyawa, Chakumba, Napamweza, Kumpata, Kuchilanga, Kuyalani.

Apr. 22, watoto 11 wa School yetu walifanywa waanafunzi majina yao; Nyamanzi, Mnatanje, Mandoli, Ng'ombo, Ntakayao, Chombo, Chikwemba, Mpazo, Mayupe, Chipenjele, Dikani. Mwezi wa May 26, Muungu akapenda kutuchukua Mr. Pearson katika dunia hii, May 27 mwili wake ukastarehe kaburini. R.I.P.

MSIMULIZI. 791

Mwezi wa May alikuja Mr. Nicoll pamoja na asikari zake, Wahindi na Wamakua, walikaa hapa kwa siku zisizo nyingi, wakaingia ndani ya mashua Ousel kwenda Bandawe. Ousel alipoenda tukasikia kama mji mmoja wa huko Bandawe alitaka kuupiga sijui kwa sababu mtwana mmoja aliyekwenda kufanya kazi Blantayre alikwiba kuko huko. Lakini walipofika huko akamwita mfalme wa hapo jina lake Amalenga, naye akaja akaambiwa akae kitako chini asitoke. Bassi Watu wake walipoona kama mfalme wao hakutokea upesi kule alikoitwa, kwani aliitwa tangu assubui wahadi jioni, wakasema kuna nini leo huko? Marra amefungwa si kwa pingu, lakini kwa macho tu. Bassi wote wakakimbia. Kwani sasa wamejua habari za vita ya Wazungu ilivyo. E. M.

Mwalimu Benedict Madalito alionekana mgonjwa wa kitwa killa siku toka mwaka jana, bassi Daktari akasema heri asisome, afathali aende pahala labda huenenda akapata afya. Akasafirishwa akaenda Chitangali akakaa kule kadri va nussu mwaka, kiisha akarejea hapa. Balli akaonekana yu hali ile ile, akaambiwa na Daktari asijaribu kusoma, bassi akaenda Mbweni kumsayidia Miss Mills kuipamba nyumba ya Kilimani. Baada ya mwezi Daktari akaonelea kheri asafiri baharini katika manuari za Kiingreza labda hewa yake itamfaa. Bassi August 9 ameingia katika merikebu ya Admeli, H. M. S. Raleigh, na siku ile ile akang'oa, amesafiri Kepi. Twatumaini baada ya nussu mwaka atarudi. Salaam. Mtg.

CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu: Uzidi kuniwia rathi kwa mistari hii michache ninayokuandikia. Wajua kama Wamasihiya wetu nuss wanakaa Mwiti, bassi Padre alienda kwao kwa njia ya Miwa, akashinda Miwa siku 2 akaendelea hatta Mwiti, nako pia akashinda siku 2, Biku ya Alhamisi akarejea. Nzige ziliwasili hapa, zilitanda mtoni mwote, watu wengi wakaenda kuziangalia; lakini hazikuthuru kitu maana vyakula vilikuwa vimeisha wekwa ghalani, zilishinda siku moja unuss.

Adam alituwasilia akitoka Masasi akienda Unguja pamoja na watoto wa Newala. Aug. 11, Archdeacon pamoja na mwalimu Y. B. Abdallah walituwasilia pamoja na watoto watano walienda kusoma Kiungani, wamerudi wawaone hali jamaa zao kwa mwezi unuss; watu wakawashangalia sana vigelegele na michezo. Aug. 18, Ijuma Archdeacon akang'oa kwa njia ya Miwa, akienda Newala.

Aug. 20, Padre Cecil alienda Makonde sehemu iitwayo Makwanjilo wanapolima watu wa mzee B. Nakaam, alienda kuangalia na kuwaona wenyeji wakaao huko akarejea. Na siku ile ile mwalimu Y. B. Abdallah aling'oa kwenda Masasi kwa njia ya Newala.

MSIMULIZI. 793

Naswi juma hii hatukuwamo mno chuoni, tulikishughulika kwa kazi za kutengeneza pahala petu tayari kwa siku kuu ya Bartolomayo, usiku palikuwa na michezo. Bassi wakiwa wakicheza kijana mmoja wa kike akaanguka akafa pale pale uwanjani akicheza, nikaitwa kutazama kwani wangineo wakithani amezimia.

Siku Kuu ya Bartolomayo tumefurahi sote. Tena ni desturi ya hapa Pasaka kufanya karamu. Bassi Pasaka hawakufanya maana hapakuwa vyakula sana. Bassi karamu ile ya Pasaka ikafanyika siku kuu hii, walianza michezo Ijuma jioni wahadi usubuhi wakaacha.

Aug. 26, Habil Malita na Kate wamepata binti.

Aug. 27, walizaliwa watoto wawili Yusuf Mteta na Rehema, na tena Francis Wemba na Nina Wemba.

Aug. 12, wakapata binti William J. Mandanda na Annetta Mandanda. Aug. 27, Mwalimu Barnaba aliwasili hapa akitoka Masasi pamoja na watoto 2, tena mwalimu Petro Sulimani akitoka Newala pamoja na watoto 3. Aug. 29, Padri Cecil pamoja na mwalimu Petro Musa na wangine waling'oa kwenda wangine kwa kucheza siku kuu, Padre ameenda angalia nyumba atakayojengewa mwalimu Gilbert Mpalila kukaa na kufundisha watoto. Tena kuwakusanya watu maana Archdeacon atakuwapo huko Juma a pili September 2, awaone. Aug. 30, Mr. Grindrod aliwasili hapa pamoja na safari iendayo Lindi kupokea mizigo ya meli.

Tunatumaini kumwone tena Archdeacon kesho, Sept. 8, akienda zake Unguja.

Sept. 4, Mzee Barnaba aling'oa hapa kwenda Lindi maana aliitwa na yule Dachi anayetawala, kumwona hali na kumwuliza habari chache za inchi, aliheshimiwa sana huko Lindi.

MSIMULIZI. 794

Sept. 8, Palikuwa na msukosuko wa vita kidogo, ulitokea pande za Kilwa wakisema kama Mwinyi Makungaya ameikata simu iendayo wahadi Dar-es-Salaam toka Kilwa, na tena anapiga Kilwa. Tena akisema ameandika barua kwa Machemba ya kusema naye aipige Lindi nami naipiga hii Kilwa tuwaondoe hawa Madachi. Bassi siku hii Lindi watu wakihangaika, wangine wakienda shamba na wa shamba wakija mjini, na ikawa ruksa killa mume wa mji awezaye kushika bunduki aende bomani atapewa na vifao vyake pia; bassi siku ile ikawa shughuli ni hiyo watu wakienda twaa selaha, na Manuari moja ilikuja kuwangojea.

Nasi tulikuwa kwa siku 4 tangu Ijuma wahadi Juma nne tukang'oa, na yule Dachi akampa mzee B. Nakaam baruti na fataki ajilinde njiani.

Sept. 5, Tukamwona mtu wa kwetu amekuja kutulaki alitukua habari ya vita, maana watu wa hapa walimpiga mtoto wa Machemba hatta kumjeruhi, bassi watu wa Machemba wakawa wanafanya shauri kuja kupigana nasi, lakini isiwepo maana walizuia na wazee wa mji, wakisema, heri tukaulize kisa nini kumpiga huyu mwana? Tena akiwa mwenyeji ameenda Lindi haya yamekuwa mambo ya watoto. Bassi siye tukawa watu wa kujihathari sana mle Mpatila maana mjuavyo ndimo wanamovizia siku zote. Baruti wakapewa watu, nasi tukaenda kama tandu hatuachani, maana ni desturi wakiwaona watu wengi na bunduki zao hawawezi kuwachokoza, kama saa 2 ya usiku tukawakuta wanne msituni nussra kuwapiga maana hawakujibu vema walipoulizwa. Ijuma Sept. 14, tukafika hapa mjini, watu wakajaa furaha sana na bunduki nyingi zikapigwa. Lakini siku hizi zimetulia habari hizi, walikuja wazee

MSIMULIZI. 795

6 wasemao magambo huko Machemba na Sultani, wawili Kangomba na Kumitema wakakutana hapa wakapatana kukata maneno, sasa twapatana kama kwanza. Lakini hazipumziki habari za vita, maana twasikia Makwangwara yapo pahali fullani, marra fullani ndiye aliyewaongoza Makwangwara yaje mijini pangu.

Sept. 18, Ndipo wakaturudia ndugu zetu 3 Samwil Sulemani na wenziwe waliopelekwa Unangu na mzee, wampelekee zawadi Che Kalanje, wamemletea pembe moja ya tembo itokayo kwa Che Kalanje kumpa mzee Nakaam.

Meli hii wanarudi watoto 4 waliokuja pamoja na Archdeacon toka Kiungani, kuwaangalia jamaa kwa muhulla, ndio Francis Sapuli, Alfred H. Mpetula, Ambrosio Mitande, Augustino Malemla. Naona mtapenda kusikia kama mwalimu Gilbert ameanza kazi yake huko Mwiti. Salaamu. A.K.

NANYANGA.

Salam kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa na inchi zetu. Msafara wetu ulitoka hapa kwenda ng'ambo ya mto Ruvuma kutafuta uchumi wa mpira. Lakini hawakudiriki kutafuta mpira, marra ikawakuta vita ya Kimavia, lakini mmoja wao hakufa illa mtoto wa mwenyewe Liumanga alikamatwa. Nao waliobaki wakarejea, na yule mtoto hakupatikana hatta leo yuko huko Mavia. Tumepata habari za vita ya Makwangwara ya kuwa wako Ruvuma, ndio Alhamisi, Ijumaa nimefunga

MSIMULIZI. 796

safari ya kwenda Newala pamoja na mke wangu. Tukawasili Newala usiku kama saa pili, nikarudi Newala pamoja na mtoto wangu mmoja, na mke wangu nikamwacha huko maana ni thaifu thaifu. Tumepata habari ya kuwa Makwangwara wanavuka leo kuja upande huu wa Rovuma kwa hawa Mangoni wakaao karibu yetu kuwapiga. Lakini tukaangalia wala hawakuja, mpaka siku ya sita Makwangwara wakavuka mto Rovuma usiku kwa usiku mpaka ng'ambo hii. Nao hawakuweza kuja peke yao illa watu Wamakonde wakaao karibu na Rovuma wakaenda kuwatwaa kuja kuwaondoa hawa Mangoni kwani wathia mno hawa. Bassi sasa tuangalie ilivyokuwa vita yao. Makwangwara hawa walikuwa wengi sana kupita kunena. Nao walijigawa kwa vikosi vitano, nao Mangoni waliposikia ya kuwa vita ya Makwangwara inakuja walikuja pamoja hatta kuwa kama mtaa mmoja, na majina ya wakuu wa Mangoni waliojenga hapa ndio Mkumba, Makacha, Manjongonda, Abdallah, Aliosi, Mambawa, Akumbota na Mkula. Bassi hawa Wafalme 8 wakajenga boma penyi ziwa la Mnyawa, maana wawe na nguvu za kuwashinda Makwangwara, nalo boma usiku hulijenga na assubui hawafungui illa kunako saa pili. Kwani huona vita haiji tena kwa leo jua linapanda. Lakini kwani killa watakapokwenda njia ya Rovuma huthani ya kuwa vita itatokea ya Rovuma kumbe wenzao wakawatokea kinyume, na mbele ya kufika kwa hawa Mangoni walijigawa vikosi vitano, kikosi kimoja kikabakia kule kule Rovuma wao kazi yao ndio kuwangojea Mangoni watakakotokea. Na kikosi cha pili kikapita mbavuni mwa kilima; na kikosi

MSIMULIZI.797

cha tatu ndio kilichopita karibu ya ziwa Iao, na cha nne ndicho kilichopita penyi boma pamoja na watangulizi wa Kimakonde; na cha tano ndicho kilichopita hapa Makonde, wao ni wa kutia alama ya kwamba vita siyo ya kuwaharibu Wamakonde illa Mangoni. Bassi mwangalie mwana wa Kingoni ginsi alivyokaa kwa ujasiri na umati wa wanaake mwenyi boma, na Mgoni akanena ya kuwa leo ndio kupigana. Haya Makwangwara wamekwenda hatta mwenyi Mkumba wakamkuta amebarizi barazani mwenyi askari wote bunduki, na kiongoni akasema, Huyu ndiye Mkumba mkubwa. Mangoni waache bassi asikari wake wapige bunduki, lakini Kwangwara akanena, burre leo sharti kumkamata mwenyewe kwanza, wakamtia mikono. Na asikari hapana hatta mmoja aliyeokoka wote wakaja papo hapo, na kule boma limefunguliwa watu wote wamo ndani baruti wanagawa; na Makwangwara wote wakaingia ndani, bassi hapo ndipo walipokuja watu wengi sana pamoja na mateka mengi sana wameteka. Tena mkubwa jioni akauawa. Nao walianza kupigana saa pili assubui mpaka saa saba tukasikia bunduki kimya, kwani hapa karibu sana na hawa Mangoni kama mwendo wa saa mbili. Na kwa vita hii Mangoni wengi wamekufa, tena wengi sithani katika wakubwa 8, kuna mmoja aliyeokoka maana vita hii ni maji wala si watu. Tena Mangoni wengi wametawanyika kwa killa uendapo katika miji huna buddi utamwona Mgoni, na Wamakonde wengi waliokuwamo vitani humu. Bassi mimi nionavyo ndio mwisho wa hawa Mangoni, na Wamakonde hupenda hawa waondoke hapa maana watu hawa waharamia, tena wanyang'anyi sana ijapo humu

MSIMULIZI. 798
hawa Makwangwara wapo. Sasa wanawatafuta popote msituni. Salaam. B. M.

KIUNGANI.

Salamu sana. Baada ya salamu, nakuarifu habari kidogo tu. August 15, wametuasilia hapa Isaya Mwalinjila na wenzake wanne watokao kutazama jamaa zao pande za Masasi na Newala.

Aug. 21, ilikuwa harusi Mbweni ya Padre Peter Limo na Blandina Mwamkwama, ilistawi sana.

Aug. 24, Siku kuu ya Bartolomayo Mt. assubui tulienda Christ Church kwa ibada ya Eukaristi Takatifu, tulipokwisha tukapewa chakula cha assubui tukarudi hapa. Lakini siku yenyewe ilikuwa Ijumaa, bassi hatukufurahiwa mno, marra tuliporudi tukaanza kuosha nyumba na kupamba tayari kwa Mkutano wa siku ya pili.

Aug. 25, Ulikuwa mkutano hapa, Mbweni na Mkunazini ilikusanyika hapa, na jioni wageni wengi Wazungu walikuja mnamo magadi. Hatta jioni ilipowaidia wageni wakarudi killa mmoja kwa maskani yake.

Aug. 27, tuliingia chuoni kusoma.

Aug. 28, ndio Siku Kuu ya Augustino wa Hippo, tulicheza siku nzima.

Aug. 29, tulifanya safari kwenda Dunga, Wazungu 3 Mr. Lister, Mr. Hitchborn na Mr. King, na watoto 34, na wapagazi 3. Tulitoka hapa saa thenashara assubui na tukawasili Dunga saa nne. Marra tulipofika tukanunua mbuzi tukamchinja, na mchele tulichukua

MSIMULIZI. 799

mwingi. Tukalala siku moja kule, Ah! siku hiyo moja ilikuwa na uhondo wake.

Aug. 30, saa kumi tukarudi zetu hapa tukawasili saa kwanza kassorobo.

Aug. 31, tulicheza siku nzima kwa ufathili tuliopewa na Askofu wa Libombo.

Sept. 1, Peter Limo na mkewe wamesafiri Bonde, na kuanza kazi yake ya Kibai.

Sept. 6, Tulianza kutazamiwa Examination kwa darasa nne tu, hatta Sept. 11 ikamalizika.

Sept. 12, tulicheza maana Examination imekwisha, bassi ndio ikawa siku ya kiinua mgongo.

Sept. 17, Archdeacon na Mr. Madan na Arthur R. Mvenya wamewasili Unguja, Archdeacon akitoka Newala, na Mr. Madan na Arthur R. Mvenya wakitokea Nyasa.

Sept. 24, Marks za Examination zilitolewa; Darasa ya kwanza: 1, Daniel Usufu; 2, Kolumba Y. Mzigala j 3, Leonard M. Kamungo. Katika darasa ya pili: 1, L. Mattiya Kangati; 2, Yohana W. Akupata; 8, W. Hilary Likwambe. Katika darasa ya tatu: 1, William B. Mpota; 2, Julius Mkonda; 3, Musa Mjema. Katika darasa ya nne: 1, Adamu Saburi; 2, Mikael Malesho; 3, Daudi Tovi. Bassi hao walioshinda walipewa zawadi zao.

Sept. 25, Jioni ilianza Retreat kwa Chama cha Paolo Mtakatifu, bassi ikawa siku nzima ya Kupriano Mt.

Oct. 2, Waliingizwa Uaalimu, L. Mattiya Kangati; Hilary Likwambe, na Edward Koongani.

Oct. 4, ilikuwa harusi ya Nicholas Kusi na Clara Kabutu, ilistawi sana.

Oct. 17, Alfred H. Mpetula aliingizwa kuwa Mwalimu.

MSIMULIZI. 800

Lakini Oct. lO, walituasilia hapa Francis Sapuli, Alfred H. Mpetula, Ambrosio Mitande na Augustino Malemla wakitokea Chitangali.

Oct. l8, Meli ya Ulaya iliwasili pamoja na Shemasi Samuel Sehoza akitoka Ulaya. Siku ile ile alifika Padre Chambers na Bwana Lister akitokea Bonde pamoja na watoto 10 wa Bonde, wanne wanakaa hapa na sita wanakaa Mkunazini kwa Mr. Lister.

October 20, tulikwenda Mkunazini kuzindua nyumba ya mabibi wa Hospital. Tena jioni siku ile ile ilikuwa karamu kwa Chama cha Paolo Mtakatifu.

October 22, Tuliwasafirisha wenzetu watatu waendao kuanza kazi ya kufundisha barra, ndio Daniel Usufu atakaa Chitangali, Kolumba, Yohana Mzigala na Karlo Edward Lisomba watakaa Newala.

Bassi Oct. 25, tulicheza siku nzima, na Ootober 26 tulicheza nussu ya siku tu.

Oct. 29-31, tumefanyiza waalimu Prize Examination. Mtg.

MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam, baada ya salaam, nakuarifu habari zetu za hapa, kama panapo Aagust 21, ilikawa harusi kati ya Padre Limo na Blandina Mwamkwama. Hatta panapo Sept. 1, tukawaaga, kwani ni watu wa pande za Bonde, wamemchukua pamoja nao Alice Mashaka, akifuatana nao mwalimu Emma Nasibu, aliyekuja kupunga hewa baada ya msiba ule mzito uliomwangukia kule ndio kapotewa na waanawe wawili.

MSIMULIZI. 801

Aug. 22, Twaliombewa na mwalimu Blandina iwe siku ya kucheza, tusisome, bassi hatukusoma, twalicheza tu hapa petu.

Aug. 24, Siku kuu ya Bartolomayo Mtume, twalikaribishwa Kiungani, bassi tukaenda, panapo jioni tukarejea kwetu. Sept. 21, Siku kuu ya Mattayo Mtume twalishinda petu tukijifurahisha na michezo yetu ya killa siku.

Sept. 29, Siku kuu ya Mikael na Malaika wote. Bibi yetu (Bibi mwalimu) alitufanyia karamu katika shamba lake, wote tulifurahiwa sana sana. Ilikuwa karamu kubwa. Alitufanyia hivi kwa ajili siku hii ndipo alipoacha kwao safari yake ya kwanza kuja kwa kazi ya Upelekwa A.D. 1879.

October 4, Ilikuwa harusi kati ya Nioholas Kusi na Clara Kabutu, walikaa Mbweni kadri ya siku 7 kwa siku kuu yao, hatta ya saba wakaenda makaoni kwao ndio katika nyumba ya Captian Agnew. Mwalimu Clara afundisha Mkunazini.

Sept. 18, Luka Mt. hatukwenda pahali twalishinda hapa hapa.

Sept. 28, Simon na Yuda Mitume twalipata nussu, kwani ilikuwa Juma apili.

Nov. 1, Watakatifu Wote, twalishinda petu hapa, lilikuwa kusanyiko la Chama cha Watakatifu wote, wakafanyiwa karamu, kiisha wakafanyiwa sala Kanisani wakaagana. Kweli nimesahau habari moja Aug. 13 jioni walibatizwa watoto hawa Faith Hoka, Ada Corale Anamema, Margaret Nelehaya, Lucy Isabela Waride, Phoebe Chiku, Rehema Yasmini. Tena imejengwa sebule mpya nzuri sana, na sasa imekwisha, Nov, 4 ilianza kutumiwa. K. Sh.

MSIMULIZI. 802

NEWALA.

Mwe rathi safari hii sina habari nyingi. Mzee Matola alimtuma Che Munomadi kwenda kupata habari ya Makwangwara. Bassi siku ya pili huyu mjumbe akarudi pamoja na Makwangwara watano, mkuu wao ni Kasembe. Hawa walitumwa na Sanangura na Chakoma na Msaka bin Sonjera; kwani huyu mtoto wa Sonjera sasa ametwaa jina la Msaka.

Bassi huyu Kasembe alitumwa kuja hapa kuomba chakula na mboga.

Mzee Matola akakusanya watu barazani, hatta baraza ilijaa kufuru, katika watu hawa, wenyi bunduki walikuwa 200 na zayidi. Bassi Mzee Matola akawaamuru majumbe ndio wafalme wadogo wadogo ya kwamba wawape Makwangwara chakula. Bassi marra hiyo ungi wa chakula kikaja kingi mno na kuku kama settini na zayidi na mbuzi wawili wakapokea Makwangwara. Lakini mbele ya kuwapa chakula, Mzee alimwambia Kasembe na wenzake; waende wakawaambie wakuu wao ya kuwa sisi urafiki wetu wa amani tupu, haifai kuomba, kwa sababu mkiwa mnatoka vitani, na sisi tukiwapeni chakula, imekuwa tunashariki vita zenu. Balli sisi tutakuwa tukiwapeni riziki mjapo kwa amani, lakini leo nawapeni maana mmekuja na mtoto wa rafiki yangu Sonjera. Kiisha akawapa chakula na watu wakawasindikiza mpaka Nangadi. Chibwana che Mbika pia alikwenda, hao kujaribu kukomboa watu waliokamatwa Wamakua na Wamakonde; na Mzee alitoa mitumba 8 kuwasayidia. Lakini hayakupatikana makombozi, kwani Makwangwara hawataki nguo, maana wenyewe wamekuwa

MSIMULIZI. 803

kama nyama hawavai nguo. Basai wakajaribu kupata watumwa wakawakomboa kwa makombozi mangine. Furaha kubwa kumpata mama yake Che Patriki, Mangame, bibi yake Silwano Ngaweje huyu mtoto anayesoma Kiungani, zamani aliuzwa Kumachelela. Bassi Makwangwara wakamkamata kwa Msaka, Mzee alipopata khabari akaenda kumkomboa, balli hamfahamu hatta mtu wa hapa ijapo huyu mwanawe, maana aliuzwa zamani.

Bassi huko Nangadi Makwangara walikaa mda wa siku 6 wakatoka. Lakini walipita ng'ambo hii ya Rovuma, na wangine 40 walipita hapa petu na ngao zao na mateka yao. Siku hiyo walipokuja ilikuwa kama vita nzima, kwani walikuwa wengi; na wakashinda hapa siku 6, wakatoka hapa Oct. 20, wamepitia njia ya Masasi.

Ilitokea safari kwenda kutwaa barua Lindi zitokazo Unguja, na mkubwa wa safari alikuwa Patriki Mangame. Bassi zamani za kurudi walipofika Mpatila, mtu mmoja wa Chitangali alitangulia peke yake mbele, Wamachemba wakamnyang'anya mzigo wake. Na mzigo huo ni kasha moja la Ulaya na gora kumi na nane za kaniki, na ndani ya kasha mna misalaba. Bassi walipomnyang'anya assubui maana alitangulia peke yake, bassi alipokutana na wenzake akawapasha habari. Bassi safari ikatua pa Mpumbe, ndipo safari ya Newala ilipolala, na wapagazi wa Chitangali walitangulia wakalala karibu na Mpindimbi.

Bassi wale Wamachemba kwa tamaa yao wakafuata tena.

Usiku watu wa Newala walipolala na bunduki

MSIMULIZI. 804

zao, kwa bahati akaamka Yona Selenje kukoka moto. Marra mtu mwingine jina lake Josiah Saadi alipoona moto kuwa mwingi akaamka kuupunguza kwani aliona itakuwa hatari. Bassi marra alipokwisha kuupunguza moto, akaona watu wanakuja na bunduki zao na pembe za baruti wamejifungia kiunoni. Josiah akatambua ni adui.

Bassi akamfinya Cbe Patriki akamwambia, kama "Ng'ondo jila ajino, nambo mwe mkasimjimuka, tinyende une jika ngausye," maana yake, Vita ile hii hapa, lakini wewe usiamke, nitakwenda peke yangu nikaulize. Bassi wale adui wakaja zao mpaka karibu pale walipolala, akaja mmoja kuhasibu watu, kiisha akawarudia wenzake, akawa akiwasimulia, marra Josiah naye akatoka na bunduki yake, walla hapana aliyejua illa Patriki, na wale Wamachemba hawakumwona yeye alipowajia wakawa wakipeana mashauri ginsi ya kupiga bunduki na kunyang'anya mizigo. Bassi Josiah akanyemelea mpaka karibu yao. Akawauliza, Nani ninyi? Kimya hawakujibu, akawauliza tena, Wasijibu; alipowauliza marra ya tatu, wakaanza kukimbia. Marra Josiah akapiga bunduki yake, akampiga mtu mmoja mgongoni akaanguka chini, akapiga ukelele wa kufa. Josiah alipotaka amwendee ammalize, naye mwenyewe akaanguka shimoni, akaja mwenzake aliyepigwa akaokota bunduki ya yule aliyepigwa akaenda nayo mbio. Bassi Josiah alipoamka kumbe yule aliyepigwa amekwisha kujikokota penyi msitu, akawa anaugua kwa sauti kubwa pale. Marra wapagazi wakakimbilia wakaona damu nyingi ziwa zima la damu.

Lakini watu wangine waliposikia bunduki ile katika

MSIMULIZI. 805

usingizi wao marra wakaondoka kwenda mbio tu kwa woga wakithani labda ni bunduki ya adui. Lakini walioamka na kukimbilia kulikolia bunduki hao ndio wanaume. Bassi Patriki akawarudisha wale waliokimbia kwa woga. Bassi wakamwacha yule mtu anaugua pale msituni, wakachukua mizigo upesi upesi wakihofu labda watakuja tena.

Wamachemba jamani siku hizi wamechaga njia ya kwenda Lindi.

Mwezi uliopita wamepigana na Chikambo, na Wamachemba walishindwa marra mbili, lakini marra ya tatu wakamshinda Chikambo, Wamachemba wengi wameuawa.

Siku hizi Chikambo yuko Lindi kwa Dachi, kaenda kutaka mzinga apigane tena na Machemba.

Tena tumesikia kama Che Makunganya amemwita Machemba amsayidie kuwapiga Madachi wanaokaa Kiswele, kwani anena si wengi huko. Bassi Machemba bin Mchakama kapeleka watu kumsayidia. Wakiisha kupiga huko wasema ataenda kupiga Lindi. Lakini wapi, wamekwisha mwacha Mdachi amejenga Mrima watamweza wapi, naye akiwa ana mizinga yake kathawakatha. Bassi tusikiavyo Makunganya alijaribu kupiga Kilwa, lakini wapi ameteketezwa watu wake wengi, ni heri asimwendee tena Mdachi, maana Mdaohi yu macho hasinzii, na vita ni chakula chake. Huzuni imetupata ya kuwa ndugu yetu mmoja amekufa, tena siku ngine alikufa mwanamke mmoja Mmasihiya tukaenda kumzika. R. I. P.

Siku hizi ilifikiriwa lijengwe kanisa jipya, balli naona haiwezekani, maana pana mnong'ono wa kuhama Malumba, mwendo wa siku tatu kufika mahali penyewe.

MSIMULIZI. 806
Na Mzee B. Nakaam naye nasikia anahama kwenda Kuchiwatu katikati ya Satiya na Mwiti, bassi kutakuwa na mabadiliko mengi. Salaam. S. Ch.

SAFARI toka NYASA hatta UNGUJA.

Kwa mkuu wa kutengeneza salamu sana, na baada nitakuarifu habari kathawakatha za safari yetu toka Nyasa Mr. Madan nami.

Tulitoka Likoma July 27 assubui na mapema, tukaingia katika s. s. 'Demira' stima ya Kampeni. Sababu stima yetu ya Mission ilikuwa ikitengenezwa mitambo kwani iliingia itlafu kidogo. Bassi tulitoka Mr. Mndan na mimi na watoto wawili wakienda kufanya kazi Zomba anapokaa balyozi wa Kiingereza, majina ya watoto Tito Kungurukutu na Simion Kristofer Mjeleka.

Siku hiyo hiyo tukafika kwa Jumbe, na mwenyewe alikufa karibu kama juma unussu tu, bassi sababu hii Mr. Nichol akaaye Fort Johnstone alikwenda huko na askari zake wa Kihindi kutengeneza habari za mfalme mwingine, watu wasifanye uthia. Mr. Madan alishuka walakini mimi sikushuka, bassi akaona maji yanachemka kama yamepikwa, hatta ukitia kiasi ao muhogo ukiutoa umeiva sawasawa, na huthubutu kutia mkono wako utaungulia mbali; minazi ipo na malimau tele tukalala hapo.

July 28, Tukatoka kwenda Fort Maquire, tukafika jioni, Ee bwana wee! mtu uliyepita zamani hupatambui kama ndipo alipojenga Che Likanje, pamebadilika sana wala mimi sikuthania kama patakuwa hivyo, licha ya

MSIMULIZI. 807

mimi hatta yeyote aliyepaona kwanza angesema kathalika.

Tukatoka July 29, saa kumi ya usiku, assubuhi na mapema tukafika mji Maganga, napo pana Mission ya Waskoch. Tdka hapo hatta Livingstonia ndiyo station ya zamani sana ya Waskott, nao umejengwa vizuri kadri; tukawakuta wenyewe wanaingia Kanisani kwani juma pili siku ile, wala mimi sikupata nafasi ya kushuka. Hatta saa nne, tukang'oa nanga tukafika Monkey Bay jina la asili Lisumbwi, hapo pana station ya Universities Mission.

Hapo tukakaa saa nzima, wakapakia kuni kwani ndiyo makaa yao, tukatoka hapo hatta saa ya kwanza ya usiku tukapita mlangoni mwa mto Shire inapoishia Nyasa tukalala hapo; kwani Domira haikuweza kufika hatta Fort Johnstone, panapo mji wa Mponda, walakini mwenyewe amekimbia milimani hataki tena kurudia mji wake.

July 30, Tukashuka katika Domira tukapita mashuani hatta pa Mponda, walakini tulipita haraka sana kwani H. M. S. 'Dove' ilikuwa tayari nayo ndiyo itakayotuchukua; hatta waalimu hao wanaokaa hapo pa Mponda hatukuwaona. Tukaenda nyuma ya forotha kupokea cheti. Tukataka saa tatu pamoja na Major Edwardes mkuu wa Wahindi, ndiye aliyepigana vita zote, alikuwa akienda kwa Ghe Kawinga Mlanje kupigana. Hatta jioni tukafika Fort Lionde tukalala hapo, kwa maana mtoni stima hatta mashua haziendi usiku kwani mafungu mengi ya mchanga zitakwama marra kwa marra. Hatta assubui July 31, tukatoka kwenda Matope panapo saa ya pili tukawasili Fort Sharpe, hapo stima ikapakia kuni, tukatoka kama nussu saa tu tukafika

MSIMULIZI. 808

Pimbi panapoundwa stima za huko walakini si zote. Bassi hapo akashuka yule Major Edwardes, Wahindi wawili na watoto wale wawili waliokuwa wakienda Zomba wakafuatana na Major Edwardes. Tukaagana nao, nami nikawa peke yangu na Wazungu wawili Mr. Madan na Mr. Mathewsy huyu mzungu alikuwa hawezi kwenda, miguu imekufa yote miwili, alikuwa akienda Ulaya Ingereza kufanyiwa dawa.

Bassi tulipotoka Pimbi tukafika Matope saa a sita tulienda upesi. Tukalala Matope siku moja unussu, napo inaundwa stima ingine ya Kampeni mpya, Murphy Makamla ndiye msimamizi wa hapo.

Aug. 2, Tukatoka kwenda Blantyre. Aug. 4, ilikuwa mashindano ya Wazungu kupiga shabaa bunduki, aliyeshinda Capt. Villiers nahotha wa H. M. S. 'Pioneer'. Blantyre ndio mji wa Wazungu watupu, tena vitu vya Kiingereza vitupu, jina lake la asili Kabula; sehemu mbili, Mission na Kampeni, tena penyi afya kwa Wazungu, Rev. G. W. Atlay alitukuta hapo akitoka Ulaya.

Aug. 6, tukatoka kwenda Katunga njiani tukakutana na mwalimu William E. Kanyopolea na mkewe na watoto wake 2, tukahuzunika sana kukutana njiani kwani hatukuweza kuongea vema naye, hatta Mr. Madan alihuzunika sana naye. Bassi tulipofika Katunga kama saa tissa, bwana wee Mtengenezaji achilia mbali siyo kunena! nzige walipita hatta jua halikuonekana nuru yake hatta kidogo saa tissa hatta saa thenashara, wala wasiishe hatta kidogo; ukitazama majani mekundu kwa nzige; Aug, 7, tukatoka kwenda Chiromo, tukaingia mashua moja wote sisi, siku 2 tukalala mtoni hatta Aug. 9, tukafika Chiromo kama saa ya kwanza u nussu, huu ndio mji uliyo mkubwa wa mitoni iliyo miji ya

MSIMULIZI. 809

Waingereza. Tukaikuta s.s. 'Lady Nyasa' tukaingia hiyo hatta Aug. 10, tukatoka nayo ilikuwa ikikwama marra kwa marra kwani maji haba, hatta Aug. 11, tukafika Msanje Fort Herald tukakuta stima mbili H.M.S. 'Herald' na s. s. 'Bruce'. Tena ikaja nyingine s. s. Jabowie, Juma a pili tukashinda hapo, nikafurahi sana kuonana na Gilbert Matengwe na Mattayo Lamilako. Tukasali pamoja nao, Aug. 13, tukatoka tukaingia katika s. s. "Bruce" hatta Aug. 16, tukafika Chinde mji ulio bandari, siku hizi nao unaendelea uzuri wake tangu kuanza ni miaka 2 tu bassi; mimi nilipopita zilikuwa nyumba tatu tu bassi; sasa hatta kuhesabu sikuweza hatta nalistaajabu ginsi ulivyostawi, na mtoni mna Kampeni nyingine inaitwa ya Sharra.

Tukakaa Chinde tangu Aug. 16, - Aug. 24, Juma nzima.

Hatta Aug. 25, tukatoka tukaingia kastima jina lake 'Union' nayo ilipigwa mawimbi kufuru, wimbi moja tangu mdomoni hatta usukanini, utathani itazama, wenyeji husema kama inafika Natal, bassi mimi nalistaajabu sana hatta moyo ukatekewa.

Tukaingia katika s.s. 'Saxon' nazo hizo zote 'Union' Stima, tukafika Kilimeni Aug. 26, wakashusha mizigo hatta assubui ya pili tukang'oa nanga kuja kusini. Tukafika Msumbiji Aug. 29, na meli tuliyokuwa tukiijia ikatukimbia, bassi tulikaa Juma nzima Msumbiji, kwa bahati yetu ikatokea meli ya Wadachi s.s. 'Setos' ikasema inakwenda Unguja, tukaingia Sept. 5, tukarudi tena Kilimeni marra ya pili, ikapakia shehena, wakati wa kurudi ikakwama marra mbili walakini ni mchangani. Tulipotoka nje maji yalikuwa yakipwa, bassi meli ikagonga marra mbili chini: toka Kilimeni hatta Wibo

MSIMULIZI. 810

tukapakia Mhebena pembe na mipila. Toka hapo hatta Mikindani wakapakia kama Wibo. Toka Mikindani hatta Lindi hapo tukakutana na Arohdeacon Jones-Bateman ni mtoto mmoja atokaye Masasi Benedikto Njewa na nikaonana na Wamasihiya wa Msumba na Pachia walikuja kuuza pembe. Toka Lindi hatta Kilwa napo hapo tulikuta vita kama wamepigana juzi Wadachi na Mahenzi mmoja Makunganya, watu wake 50 wakafa, tukasikia tena kama stima imezama siku 4 zimepita. Toka Kilwa hatta Dar-es-Salaam tukashuka kuabudu katika kanisa la Kifransa, ilikuwa Juma a pili Aug. 16, siku hiyo hiyo hatta Bagamoyo tukalala hapo. Hatta Aug. 17 saa a tatu tukawasili Zanzibar, wote salama, ilikuwa furaha sana kuonana na ndugu zetu salama salimini. A. R. M.

HABARI ZA UGANDA.

Tunafurahi kusikia kama inchi ya Uganda inazidi kutulia. Hapana hofu ya vita siku hizi. Na Kanisa la Masiya linaeneaenea zayidi killa siku. Tumeambiwa siku hizi na Askofu wao alipopita Unguja kama katika mji mkuu wa Uganda, ndio Mengo, wamekuwa Wamasihiya wengi wenyi moyo mpesi sana kuongoa ndugu zao. Bassi watu wengi walio maarufu katika Wamasihiya huko Mengo walifanyana mashauri mwaka huu wakinena, miji mingi ya inchi yetu hawana waalimu lakini wa tayari kufundishwa; bassi tumwombe Muungu kwa bidii, tukajaribu kutafuta huku mjini watu 100 watakaokuwa tayari kujitoa kwa Muungu kushika kazi ya kufundisha ndugu zao;

MSIMULIZI. 811

tukawapeleke kwa miji 100 inayozunguka mji wetu. Bassi wakaomba, wakatafuta, na Muungu aliwatia moyo watu wengi kusema 'Mimi hapa nipeleke mimi.' Bassi walitimia watu 100! Bassi watu hawa walikuwa tayari kuacha shughuli zao waende watakakotumwa, pangine safari ya siku moja mbili, illi wakae wakafundishe watu. Na walioanzisha shauri walisema 'Enyi ndugu zetu, mnaokwenda kupelekwa, gharama ya nguo zenu kwetu sisi hapa Mengo, tutakusanya mapesa yetu na kuwalipeni. Kwani walitaka rupia mbili tu mwezi. Na tena chakula chao juu yao watakaofundishwa nao. Nao pia tayari kutoa, kwani malaji na malazi na mavazi ya wale waalimu 100 sawa sawa na wao wanaowakaribisha, bassi si vigumu kuwapatia vyote. Na yote hayo yametendeka pasipo msaada wo wote wa mali itokayo kwa Wapelekwa Wazungu. Hivi neno la Muungu linakua na kupata nguvu.

NEWALA.

Kwa Mtengenezaji. Salamu baada ya Salamu nakuarifu habari kidogo za barra Newala. Ule mgogoro wa Makwangwara sasa umekwisha, na watu wamestarehe sasa, karibu killa mahali sasa watu wameshuka chini kulima, na wangine wamehama juu kabisa wanakaa chini, maana sasa shwari. Na ile shauri ya Mwenyi Matola ya kuhamia Marumba sasa amebrai sijui hatimaye.

Vita ya Makwangwara ya mwaka huu imeleta matata mengi.

Kwanza tangu kuja vita watu hawakuwa na nafasi ya kulima, kwani killa mtu akithani inakuja mjini pake, bassi wasilime illa kuhangaika tu. Hatta zamani walipoondoka Makwangwara watu wakakumbuka kazi ya kulima kumbe ni wakati wa mvua, bassi watu wameshangaa hawajui la kutenda. Afathali waliolima chini wamediriki kidogo, kuliko waliyoanza kulima Makonde.

Tena siku hizi kuna msukosuko wa zile pande hizo zote walikopiga Makwangwara. Kwani Mangoni wanasema kama sisi vita hii asingetupiga illa Watmakonde ndio waliokwenda kuwaleta Makwangwara na

MSIMULIZI. 813

Mchipili, na Namakoma, hao ndio wafalme wa ng'ambo ya pili ya Rovuma.

Bassi Mangoni wanasema, sisi mwaka huu hatukulima, kwa kuwa mlituletea vita, bassi na ninyi hamlimi. Tena sisi wake zetu tumenyang'anywa, na ninyi wenu mnao, bassi mtaona. Ndio ghasiya iliopo siku hizi hiyo. Lakini marra nyingi wao Mangoni hushindwa, balli hawakubali.

Nov. 3, Amewasili hapa Mwalimu Kolumba kuja kufanya kazi yake hapa pamoja na Mwalimu Carlo.

Ule mgogolo wa Mpatila hatta sasa ungalimo. Hapana wanaopita Mpatila mikono mitupu siku hizi, ao kumi, hamsitashara tu, illa wengi pamoja na selaha zao.

Tena Wamwera wote wanaokaa Ukredi wengi hawapo wamekimbia, wala si hao tu illa tangu Ukredi hatta Ngulumahamba watu wote wamekimbia wamebaki wachache, wote wanamkimbia Machemba Bin Mchakama. S. C.

SAFARI TOKA KOROGWE, MAGILA, TANGA, HATTA UNGUJA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari kidogo tu.

Oct. 11, Tulitoka Korogwe safari kubwa ndio Bwana Lister, na watoto wa Korogwe watatu: Samwil Kiwayo, Charles M. Mgaya na Lugula. Tena na mtoto mmoja aliyefuatana pamoja na Bwana Lister, jina lake Patriki Kiaka, na mtoto mmoja wa Magila, John. J. Mbaruku.

Bassi safari hii yote tukaenda hatta jioni tukafika

MSIMULIZI. 814

kwa Mkului, mji anaofundisha Granville Kachipumo. Assubui tukatoka tukaenda hatta tukawasili Magila.

Nyuma yetu akatufuata Padre Chambers pamoja na watoto wake wanne: Herbert H. Kidungwe, Edward M. Nyange, Samwil C. Kobo na Henry C. Sangoda. Padre Chambers anakwenda zake Ulaya maana mgonjwa.

Oct. 14, Tukatoka Magila tukafika Msaraka, na Mr. Roberts alitusindikiza mpaka Msaraka pamoja na watoto wawili. Lakini katika safari yetu tulifuatana na mtoto mwanamke jina lake Mary Pili, anashuka Unguja, akakae Mbweni azidi kusoma.

Tulipotoka Msaraka tukafika kwa Jumbe Mtondoo, ndio kati ya Bonde na kufika pwani.

Bassi sasa naona mtapenda kusikia habari iliyo ajabu upande huu wetu wa watu weusi. Siku hiyo tulipofika kwa Jumbe Mtondoo, marra tukasikia mshindo wa bunduki nyingi hatta tukashindwa kuhesabu. Marra hiyo tukamwona mtumishi wa Dachi akawaita Bwana Chambers na Bwana Lister; tulipotupa macho mbele tukaliona gadi la moshi kubwa sana, na limefungasa magadi mangine zayidi ya sita.

Tena tukaona umati wa Wazungu na watumishi wao. Bassi tukauliza, kuna nini leo? Tukaambiwa, leo ni karamu ya kufunguliwa njia hii ya gadi la moshi, na hili ni mojawapo bado la pili kuja, hili ni la Wazungu na hilo litakalokuja ni la watu weusi. Alipotuambia vile marra twasikia ngurumo ya gadi, marra hili hapa limejaa watu zayidi ya 300 wanatoka Tanga. Na katika siku hiyo balyozi wa Unguja pia alikuwapo. Tukakaa pale kwa Jumbe Mtondoo mpaka saa nane

MSIMULIZI. 815

unussu, tena Wazungu wakaingia katika gari lao wakafika Tanga saa kenda, kwenda kwa miguu tangu pa Jumbe Mtondoo hatta Tanga ni mwendo wa saa tano, wallakini kwa gadi hutwaa nussu saa tu. Na sisi tukaingia katika gadi la watu weusi saa kenda unussu tukafika Tanga saa kumi. Nakuambia ni ajabu mno, na ginsi linavyokwenda kassi, mtu anaona kizunguzungu. Bassi linakwenda kwa kishindo kikubwa kama kishindo cha magadi I2 ya frasi yakipita karibu yako njia kuu, kathalika na kivumbi cha gadi hilo.

Njia hiyo inatengenezwa mpaka Kilimanjaro. Kiisha tukaingia ndani ya meli ya Kidachi tukawasili Unguja. J. J. M.

LIKOMA.

Salamu kwa Mtengenezaji wa Msimulizi. Baada ya salamu nakuarifu habari chache ndizo hizi.

August 25, Siku ya Bartolomayo Mtakatifu, assubui saa kwanza ilikuwa ibada kubwa ya Eukaristi Mt. Tulipotoka kanisani watoto wa chuoni na watu wa kazi walipewa ruhusa kwenda kwao kuwatazama jamaa zao; watoto wa Mchizumulu walikwenda Chizumulu, na wa ng'ambo walikwenda ng'ambo. Lakini watoto wa Msumba, na Pachia, na Chisanga ndio hawakwenda kwao, maana kwao ni mbali ati, bassi walishinda papa hapa. Siku ile ile alituasilia Mwalimu William E. Kanyopolea pamoja na mkewe na watoto wake wawili. Aug. 26, Archdeacon Maples alikwenda kwa Kotakota kwa Jumbe kuuliza kwa Mr. Nicoll, kama,

MSIMULIZI. 816

Inawezekana Wapelekwa wetu wa Universities kuanza kazi kule ya kufundisha, ao wapelekwa wa Skotchi watafundisha kule? Bassi Mr. Nicoll akajibu ya kwamba, Wapelekwa wetu wa Universities waende kukaa kule. Balli alisema ngojeni kwanza mpaka amilikishe mfalme mwingine mahali pa Jumbe. Bassi mfalme wa siku hizi ni kijana tu; naye mfalme huyu kaitikia kama vyombo vyake vyote havitatumika kwa biashara ya watumwa. Tena kaahidi katika vyombo vyake vyote Waingereza waweke asikari wa kutazamia kazi hii watu wasipakie tena watumwa.

Siku moja ilitoka safari ya Mr. Williams pamoja na wapagazi 40 akienenda Unangu, lakini njiani usiku walipolala, alikuja mwivi akaiba mtumba mmoja, na sanduku moja la majembe; Na mwivi huyo jina lake Makwinja, kwake ni Chisindo. Aug. 31, alituasilia Mr. Butler akitoka Unangu pamoja na wapagazi wale aliofuatana na Mr. Williams, tena aliwasili nao mtoto jina lake Lewis Mnjema alikuwa akikaa Unangu.

Sept. Padre Sim na mwalimu William E. K. na Sulemani Kandamupamoja na mkewe Zoe Kusingati wamekwenda kwa Jumba. Sulemani K. aenda kupika, na Mwalimu William Edward E. aenda kujenga nyumba yake. Siku ya pili yake zilituasilia Manoari mbili za Waingereza, H. M. S. Advanture, na H. M. S. Pioneer, watu wa kisiwa hiki Likoma waliogopa mno, wakawa wakiulizauliza, jamani kwani manoari hizi zimekuja Likoma? Ah! bwana manoari hizi hazikujia vita illa matembezi tu. Mkaona wapi Sultani asiyetembea kutazama miliki yake, bassi hizi manoari zimekuja kuangalia Likoma. Bwana Archdeacon

MSIMULIZI. 817
amembatiza masikini mmoja jina lake Mary Mantisewa. Tena Dr. Robinson kaenda Ulaya Uingereza kupata afya, maana alikuwa hawezi vidonda, akijaliwa tunatumaini atarudi tena. A. T. M.

MAGILA.

Nakuarifu habari chache tu. Siku hizi imekunya mvua kubwa sana, killa siku mvua tu. Hatujaiona mvua nyingi kama hii kwa miaka mingi, hatta ukitaka kusafiri huko na huko ni kwa shidda nyingi. Huna buddi kuogelea mitoni, maana mito yote imejaa maji, na utauthika mno kwa matope hatta nguo zako hazitamaniki tena. Wallakini, haithuru maana jua liliwaka mno mwaka huu, bassi tukaomba dua kwa Muungu atushushie mvua, bassi Muungu ametusikia haja yetu. Tena kuna habari mbaya zimetokea katika inchi ya Bonde, naona mlisikia kama nzige zilifunikiza inchi yote pia, wallakini tena zikatoka zikaenda zake. Wallakini mwezi huu tena zimerudi nzige nyingi sana, wamekula makonde yote ya chakula kilichoanza kumea, bassi sasa imeangukia njaa tupu katika inchi ya Bonde. Tunatumaini tutasayidiwa kwa sala na sadaka za ndugu zetu wangine. Tulisikitika sana kwa sababu Bwana Askofu wa Mombasa hajafika huku. Amekusudia aje hapa Magila apatazame, na kuwatia watu mikono, na kumwamuru Mr. Kisbey katika daraja ya Ukasisi. Tumesikia kama ana homa huko Unguja, bassi Mr. Kisbey anashuka huko Unguja apate kupokea daraja yake ya Ukasisi. Dr. Palmer amewasili Bonde. George Swedi anafanya kazi hapa Magila.

MSIMULIZI. 818

HABARI ZA UGANDA.

Tunafurahi kusikia kama inchi ya Uganda amani tupu. Bassi tumepata barua ya Uganda inaeleza zayidi hivi.

July l, Tulifurahi sana, kwa sababu tulisomewa hati ya Ulaya Ingereza, bassi mkubwa wa Government akasema, ameletewa barua ya kusema kama, Queen Victoria amekwisha kukubali kutwaa Uganda kuilinda dayimara, na kuwaweka askari zake wakae huku.

Bassi nasi Waganda tunapenda sana iwe amani pote na tuliposikia maneno haya tulifurahi mno, hatta tulipiga bunduki siku nzima. Kwa sababu sisi tunajua kama Wazungu wakiondoka katika inchi yetu, sisi na hawa jamaa zetu tutapigana marra; kwani walitumaini kama Waingereza wakitoka inchi yetu, tupigane tena wapate kutufukuza Uganda, wakae peke yao tu.

Zamani twalikuwa kama Wayahudi siku zile walipogombana wao kwa wao, wasipatane vema, ndipo Tito akaja akawapiga marra moja. Kathalika na sisi tusipopatana wenyewe kwa wenyewe, pangine huenda likaja jeshi la Islamu na kutupiga marra moja.

Tena inchi ikiwa na amani watu wanaweza kwenda mahali hapa na hapa kufundisha habari za Anjili ya Bwana.

Siku hizi watu wengi wamekwenda kufundisha mahali pangine pangine pa inchi yetu, na walioenda kutenda kazi zayidi ya 100, ao labuda 115, ao 116, ao 117. Lakini niwajuao ni 109, na tena wameongezeka, kwa sababu wanakwenda killa siku wala hawajulikani vema.

MSIMULIZI. 819

Tena tumefurahi mno kumwona ndugu yetu Charles William Rehani na mkewe Hope B. Rehani, waliwasili hapa Mengo June 10.

Tena tunaomba sana tupate Bible kwa lugha ya Kiswahili; kwani tumepata habari kama itapigwa chapa huko Ulaya, tena tunatumaini kupata English Swahili Dictionary.

Bassi shukrani tumpe Muungu, kwa sababu Neno lako linazidi kukua katika inchi ya Uganda; tena tuzidi kumwomba Muungu aamshe mioyo ya Waganda na Afrika nzima, ilipokee Neno lake lenyi Nuru, giza yote iondolewe mioyoni mwao.

Ee Bwana Mkuu wa Mavupo, uwajalie Wamasihiya Waafrika wasiwe na choyo kwa elimu ya Anjili, illa wawahurumie makabila ya Afrika wasiyojua bado kweli ya Anjili, illa wawatakie sana njia ya wokovu wako.

Tena kwa nyuma zimekuja barua za kusema kama Kanisa lile kubwa la Mengo waliolijenga la miti mikubwa sana limeangushwa na tufanu. Likaweza kuchukua watu 4000 ndani yake, na miti yake mikubwa ilikwenda kukatwa msituni mayili 30 kutoka Mengo, ikataka killa mmoja wachukuzi 200. Kanisa kubwa ajabu hatta lilipoanguka hakuwamo mtu. Ndani yake huenda watu 3000 killa assubui kusali, Juma apili zayidi. Mahali pake watajenga Makanisa mawili kwani hili halikutosha.

MSIMULIZI. 820

KIUNGANI.

Safari hii naja kwako kwa maneno machache tu, maana sina wa kunisayidia kutia shime nipate niwe na habari nyingi. Bassi huu ni mwisho wa mwaka, tutaonana tena mwaka mwandamo.

Padre Simpson alisafiri kwenda Kepi kupumzika kwa mwezi mzima, baada ya mwezi amerudi tena hapa.

Tena Mwalimu Archibald A. Semmanyi alienda Mkuzi kumchukua mkewe, naye amerudi pamoja na kitoto chao jina lake Herbert Woodward.

Nov. 25, tulipamba nyumba yetu kwa bandera nyingi, na uwani tukapamba kwa majani ya miembe na makuti; na tukatengeneza mchezo wa Vitali tayari kwa keshoye.

Labda wangine watauliza, kwa nini kupamba nyumba? Bassi nitawaelezeni.

Bassi kwenyi mwaka 1884, Archdn. Jones-Bateman alifunga safari ya kukaa hapa, kuwa bwana mkubwa wa Kiungani; bassi tangu mwaka ule 1884 Nov. 26 hatta mwaka huu 1894 Nov. 26 imetimu miaka 10. Bassi siku kuu hii ilikuwa ya kumshukuru Muungu, maana amemjalia kukaa hapa miaka 10.

Nov. 26, Assubui tulipotoka kanisani, tukakaa hatta mnamo saa tatu unussu kengele ikapigwa, watoto wote wakasimama mstarini na vitabu vya nyimbo za kufurahisha watu nyimbo za ilmu dunia.

Marra akatokea Archdeacon na kikaletwa kikapo kimejaa pesa tupu, bassi akatugawia killa mmoja bahashishi yake, wasomaji waalimu na watoto wote

MSIMULIZI. 821

wakapewa killa mtu zawadi yake. Kiisha tukamshukuru kwa zawadi yake aliyotukarimia.

Na tukaimba nyimbo za ilimu dunia, ndio mwisho. Bassi siku hiyo ukapikwa wali wa pilao, ndio chakula chetu cha mchana, tuliupiga siku hiyo wali hatta tukautazama kwa macho tu. Tena walikuja Wabondei watano walicheza mchezo wao; killa mtoto alifurahiwa mno, kiisha wakaenda zao! na Bahashishi yao. Sala ya jioni ilipokwisha, tukawa watu wa kuwatazamia wageni, marra wakaja wageni wa Mkunazini na Mbweni na Shangani, weupe kwa weusi, walikuja kutazama mchezo wa Vitali.

Vitali alikuwa Arthur R. Mvenya, Masachio alikuwa Clement Kathibeni, na Liwali alikuwa Yohana Hamisi; Ah! mchezo ulistawi. Kiisha wageni wakarudi kwao.

Nov. 30, Siku kuu ya Andrea Mt. ibada zilikuwa za shangwi sana, balli wengi wenu mnafahamu kama mwaka jana siku ya leo hivi, palikuwa kusanyiko kubwa la watu wa zamani waliokaa hapa. Bassi mwaka huu ni kathalika ulikuwapo mkutano wa Watu wa zamani, balli haukufanyika siku ile ile maana ilikuwa Ijumaa, bassi karamu ilikuwa siku ya pili yake Dec. 1, Wallakini watu hawakupatikana wengi, watu 50 tu, maana wengi hawapo wamesafiri mbali mbali, bassi kwanza tulienda kanisani. Archdeacon aliwatolea khutuba, kuwaambia kama Bwana wetu anatuambia, "Sinyi mlionichagua, illa mimi nimewachagua ninyi." Tena ginsi Muungu alivyotupenda, na amjua killa mmoja, labuda wangine wataona mambo mengi ya Kiungani mageni matupu

MSIMULIZI. 822

lakini Bwana wetu ni yule yule mmoja jana, juzi leo hatta milele. Tena tangu kuanza school ya Kiungani wametoka watoto 370, na waliofariki zayidi ya 100. Bassi killa mtu akirudi kwake amwombe Muungu ya kuwa amechaguliwa naye kati ya makafiri wengi, kuwa mtu mbele yao kwa kuwaonyesha yalio bora. Kiisha khutuba tukaendelea kwa ibada ya shangwi ya kuandamana. Tulipotoka kanisani, wakaingia mezani wakala wali wa pilao, kiisha tukaenda uwani kuwaonyesha mchezo wa Vitali, waliupenda sana. Kiisha tukawaaga wakaenda zao.

Tena tumempata schoolmaster mwingine jina lake Mr. Prior.

Alban Njengune amerudi Unguja ndani ya manoari H. M. S. Racoon akitokea pande za Kepi.

Dec. 4, Mr. Mallender amerudi akitokea pande za Newala pamoja na Samwili Chiponde na Yustino Mkandu wamekuja kutaalamu zayidi wakitazamia Daraja ya Ushemasi.

Kweli nimesahau neno moja ndilo kama, sisi wa Chama cha Paolo Mtakatifu, tumefurahiwa mno kuona kundi letu linazidi, maana Dec. 1 tumefurahiwa kumwona L. Mattiya Kangati akiingia katika Chama. Tena tumefurahiwa mno kwa John B. Mdoe kurudishwa tena katika Chama cha Paolo Mtakatifu. Mtg.

MIWA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salam. Baada ya salamu nakuarifu habari zetu za siku nyingi kidogo. Siku hizi watu wenyeji wa inchi wamo katika kazi ya kulima na kupanda, kwani mwaka huu mvua imestuka upesi kuliko mwaka jana. Tena tulikuwa, na msukosuko

MSIMULIZI. 823

Wa habari za Makwangwara wakati walipokirudi toka ng'ambo ya mto Ruvuma; kwa vita yao, bassi tukawa watu wa kujihathari ya kuwa labda huenda wakapita kwa njia hii. Lakini hayakutokea tulivyokuwa tukithani kwani wao Makwangwara walipita upande mbali kabisa nasi kwenda zao Umakwangwarani. Nasikitika ya kuwa habari nilizoandika mwezi September zimepotea njiani, katika huo naliwapasha habari ya kuwa watu kenda walifanywa Waanafunzi. Waume watano na waanake wanne.

Habari za hali ya mafundisho ya Kimasihiya watu wa Miwa wanadumu sana; jumla ya waanafunzi wote tangu upelekwa ulipowajia mwaka 1890 pamoja na Wamasihiya hesabu yao 26, kwani wajua wote ya kwamba zamani alikaa pale mtu kama mtoto Mmasihiya kuanzisha tu kuwafundisha watoto wadogo mpaka siku nyingi kidogo akaja mwalimu; yeye hufundisha wadogo na wakubwa pia. Na tena ya kuwa kazi ya kufundisha maneno ya Muungu kwa makafiri na kazi ya kuchimba na kuvunja mawe magumu ao kutoboa mwamba, si kama penyi matumbawe mengi na kukusanya marra fungu zima; si kama hivyo kazi ya kweli ya Muungu, labda kiislamu. Ukiwafundisha makafiri kuacha panya na nguruwe na nyama aliyekufa kibudu, huenda akayakubali hayo upesi kuliko kuacha matendo maovu kabisa anayokataa kukubali Mmasihiya kama alivyofundishwa na Muungu, wanayoyaona makafiri ni mambo ya anasa na kujifurahisha.

Wale niliowataja hesabu yao nimesema Waanafunzi na Wamasihiya, watu wangine wasikiaji (hearers) ndio wengi wanaokuja siku za Juma a pili na siku za mafundisho. Salamu. Y.M.